epaper.ippmedia.com
Nipashe
MIAKA 30
Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Januari 27, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581934
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Taka za plastiki janga

• **Wananchi** hatarini, ng'ombe anapofanyiwa upasuaji, kilo tano za plastiki zinatolewa tumboni...

*Endelea ukurasa 2*



Mmoja wa waokota chupa za plastiki mitaani akiwa kwenye majukumu yake mjini Morogoro hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 10

**Hospitali** ya Rufani ya Mkoa yaanza upasuaji wa ubongo

UKURASA WA 18

**Kauli** ya RC Dar yazua jambo, TLS na LHRC waibuka



UKURASA WA 18

**Maelfu** kunufaika, kampeni msaada kisheria ya Samia yazinduliwa Katavi



UKURASA WA 21

**MBAPPE: NATAKA UBINGWA WA LALIGA SI MFUNGAJI BORA**

## MKUTANO WA NISHATI



Traoré Samia Hichilema Tshisekedi Ruto

# Ikulu yaagiza watumishi wafanyie kazi nyumbani

UK. 3

# Nyuki wavamia shuleni na kujeruhi wanafunzi, walimu

UKURASA 8

**MICHEZO** **RAMOVIC APATA PAKUZUNGUMZIA** UK.24

**KATUNI** UK.6

RIPOTI MAALUMU

Na Mwandishi Wetu, MOROGORO

# Taka za plastiki janga

WAKAZI wa manispaa wako hatarini kukumbwa na maradhi, ikiwamo saratani kutokana na kukithiri kwa taka za plastiki zisizorejelezwa.

Hatari hiyo haiko kwa binadamu pekee. Wataalamu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameonya kuwa mifugo nayo inaangamizwa na taka hizo; wanapomfanyia ng'ombe upasuaji, wanatoa tumboni kilo nne hadi tano za taka za plastiki.

Ni baa lililobainika katika Manispaa ya Morogoro, mkoani Morogoro. Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), mahali hapo ni umbali wa Km 259 mashariki mwa Makao Makuu ya nchi, Dodoma.

Hii ni manispaa yenye jumla ya wakazi 471,409. Kati yao, wanawake ni 244,592 na wanaume ni 226,817 (Sensa ya Watu na Makazi, 2022). Wataalamu wa afya na mazingira wanatoa hadhari kuwa idadi hii ya wakazi na majirani zao, wako hatarini kukumbwa na maradhi kama vile saratani, kuhara, homa ya matumbo na maradhi ya mfumo wa upumuaji kutokana na kukithiri kwa taka za plastiki zisizokusanywa na kurejelezwa katika manispaa hiyo.

Kaimu Mkuu wa Kitendo cha Udhibiti Taka Manispaa ya Morogoro, Hezron Ligala anabainisha kuwa kati ya tani 377 za taka zinazozalishwa kila siku ndani ya manispaa hii, asilimia saba hadi 10 ni taka za plastiki. Hii ina maana kwamba tani 26.39 hadi 37.7 za taka za plastiki huzalishwa kila siku katika manispaa hii.

Hata hivyo, Ligala anasema ni asilimia nane tu ya taka zinazozalishwa katika manispaa, ndizo hukusanywa na kurejelezwa. Hivyo, tani 247 za taka hubaki mitaani kila siku na kuwaweka hatarini kiafya wananchi na mifugo dhidi ya taka hizo.

Katika uchunguzi wake, mwandishi wa habari hii amebaini kuwapo mrundikano wa taka za plastiki katika maeneo mbalimbali ya manispaa hii. Hayo ni pamoja na sokoni Mawenzi, Soko la Chifu Kingaru, Sabasaba na stendi ya daladala Mafiga iliyoko nje kidogo mwa mji wa Morogoro.

Mwandishi pia amebaini taka za plastiki zinatupwa katika Mto Morogoro unaoanzia maeneo jirani na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo. Mto huo hupeleka maji Mto Ngerengere ambao ni sehemu ya vyanzo vikuu vya maji ya Mto Ruvu unaotegemewa na wakazi wa Pwani na Dar es Salaam kupata maji.

Kukiwa na ushuhuda huo, Kaimu Mkuu wa Udhibiti Taka, Ligala, anataja maeneo yanayozalisha taka za plastiki kwa wingi katika manispaa hii yanajumuisha masoko, maeneo ya biashara ya vyakula, vinywaji na kumbi za starehe.

Kuepuka madhara yatokanayo na taka hizo, Ligala anasema uongozi wa Manispaa ya Morogoro umekuwa unachukua hatua mbalimbali kudhibiti uzalishaji taka za plastiki.



Eneo linaloitwa Bwaro la Umwema katika Manispaa ya Morogoro zinakokusanywa taka za aina mbalimbali ambalo lilipaswa kuwa limezungushiwa uzio kama Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) inavyoelekeza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Hatua hizo, Ligala anasema zinajumuisha kusimamia utekelezaji Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na Sheria Ndogo za Afya na Mazingira za Manispaa ya Morogoro.

Katika hili la usimamizi wa sheria, Ligala anafafanua: "Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 (kifungu cha 4(1)) inatuelekeza tusimamie haki ya kila mtu anayeishi Tanzania kuwa katika mazingira safi na salama kiafya.

"Hivyo, kitendo cha kuwapo mrundikano wa taka, zikiwamo hizi za plastiki, ni ukiukwaji sheria unaohatarisha mazingira na maisha ya watu," Ligala anasema.

Anakiri tatizo la mrundikano wa taka za plastiki katika manispaa yao ni kubwa, akieleza kuwa dosari hiyo imekuwa mtihani mgumu kwao kuitatua kutokana na uwezo mdogo wa manispaa kukusanya taka na kuzirejeleza.

"Tunawashukuru watu ambao wameamua kujiajiri kwa kukusanya chupa za plastiki mitaani. Tatizo la taka katika manispaa hii mara kadhaa limekuwa linalalamikiwa na wananchi. Hii inatokana na wazabuni waliopewa jukumu la kuzoa taka mitaani kuacha kazi.

"Wazabuni wanatukimbia kutokana na ada ndogo ya taka inayokusanywa kila mwezi kutoka kwa wananchi," anasema Ligala na kufafanua kuwa awali manispaa ilikuwa inakusanya Sh. 1,000 kwa kila kaya kwa mwezi.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Manispaa ya Morogoro ina kaya 133,809 zenye wastani wa wakazi watatu hadi wanne kwa kaya. Hii ina maana kwamba, kila mwezi manispaa inaweza kukusanya Sh. milioni 133.809 kutoka kwa wananchi kama tozo ya taka ikiwa kila kaya italipa Sh. 1,000.

"Kutokana na hali hii, manispaa imeamua kutunga Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 iliyoanza kutumika hivi karibuni baada ya kuona kuwa sheria iliyokuwapo awali haikidhi mahitaji na hivyo kuhatarisha maisha ya watu na viumbe hai wengine.

"Tulikuwa na sheria ndogo ya mwaka 2005 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2010 na 2019, lakini baadaye mwaka huu imeonekana kutokidhi mahitaji ya sasa. Awali kila kaya ilikuwa inatakiwa kulipa Sh. 1,000 kwa mwezi kwa ajili ya taka, lakini fedha hizo zilionekana kutomudu gharama za uondoshaji taka katika manispaa.

"Wazabuni walitukimbia na kusababisha mrundikano wa taka kwenye maeneo mengi mitaani. Ninaamini sheria mpya ya mwaka 2024 itatusaidia kuweka mazingira yetu salama. Sasa kila kaya inatakiwa kutoa Sh. 3,000 kila mwezi kwa ajili ya uondoshaji taka," Ligala anasema.

Hata hivyo, Ligala anafafanua kuwa wakati ada ya taka ikiwa Sh. 1,000 kwa kila kaya, manispaa ilikusanya wastani wa Sh. milioni 40 kwa mwezi, na sasa wanakusanya wastani wa Sh. milioni 100 kwa mwezi.

Ni hali inayoonesha kutokuwapo ufanisi katika ukusanyaji mapato katika manispaa hii. Kwa kaya 133,809 zilizopo (Sensa 2022), manispaa ilipaswa kukusanya Sh. milioni 133.809 kwa mwezi kipindi ambacho tozo za taka zilikuwa Sh. 1,000 kwa kaya na sasa inapaswa kukusanya Sh. milioni 401.427 kwa mwezi kupitia tozo mpya za Sh. 3,000 kwa kila kaya.

Rashid Omary (47), mkazi wa Nanenane, Manispaa ya Morogoro, analalama kuwa licha ya ongezeko la tozo za taka, uondoshaji taka katika manispaa yao hauridhishi.

"Licha ya ongezeko la tozo kutoka Sh. 1,000 hadi 3,000 kwa kaya linalotuumiza wananchi, hasa tulio na kipato cha chini, bado taka hazizolewi kwa wakati na hivyo kuwapo mrundikano wa taka mitaani," Omary analalama.

**MADHARA YA TAKA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Clement Lubeya anasema mrundikano wa taka, mbali na kuchafua mazingira, pia huzalisha hewa mbaya ambayo ni hatari kwa maisha ya binadamu.

Dk. Lubeya anasema mrundikano wa taka husababisha uozo unaozalisha na kuvutia wadudu wanaoeneza magonjwa mbalimbali ambayo ni hatari kwa binadamu, yakiwamo ya mlipuko, fangasi na minyoo.

"Uchafuzi wa mazingira ni hatari kwa afya ya binadamu. Kwa kawaida mwili wa binadamu hutoa hewa chafu na kuvuta hewa safi, hivyo kitendo cha kuishi au kupita eneo lenye mrundikano wa taka ni hatarishi kwake kwa kuwa huvuta hewa mbaya ambayo huathiri mfumo wa upumuaji," Dk. Lubeya anafafanua.

Bingwa huyo anasema taka za plastiki ni hatari zaidi kwa kuwa haziozi haraka, akitolea mfano chupa za maji ambazo kuzagaa kwake mitaani kunaweza kusababisha mitaro ya maji kuziba na hivyo kusababisha mafuriko.

"Chupa cha plastiki zikiziba mitaro, maji hupoteza mwelekeo wake na hivyo kuingia mitaani na kwenye makazi ya watu. Hicho kinakuwa chanzo cha magonjwa ya mlipuko, ikiwamo typhoid (homa ya matumbo) na kuhara.

"Chupa za plastiki kuna wakati huziba miundombinu ya maji taka na kusababisha kero kwa wananchi. Hii ni hatari kwa binadamu kwani ni rahisi jamii kuathirika kwa magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu," Dk. Lubeya anafafanua.

Ana angalizo lingine, akisema amebaini uzoaji taka mjini humo haufuati kanuni za usalama kiafya; baadhi ya magari yanayotukumika kukusanya na kubeba taka mitaani, yanaangusha taka hizo mitaani, hasa barabarani na hivyo kufanya taka za plastiki kuingia mitaroni, hata kuifikia mito mikubwa.

**WATAALAMU SUA**

Daktari wa Mifugo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Esron Karimuribo anasema madhara ya taka za plastiki hayaishii kwa binadamu pekee bali pia huathiri mifugo inayokula taka hizo.

Prof. Karimuribo anasema taka zote za plastiki huathiri mifugo, akiwatolea mfano ng'ombe na mbuzi ambao hula na plastiki zinazochanganyika na majani au nyasi. "Taka hizi za plastiki zikiliwa na mifugo, huziba mfumo wa kumeng'enya chakula na kuleta changamoto ya kiafya kwa mifugo husika. Taka hizi pia husababisha vimelea vya magonjwa na kuathiri mifugo na wakati mwingine husababisha vifo kwa mifugo husika," Karimuribo anafafanua.

Mtaalam huyo anasema SUA ina hospitali yake kwa ajili ya utafiti wa mifugo, akiwa na ushuhuda wa kinachojiri hospitalini huko kwamba: "Pale mfugo (ng'ombe) upofanyiwa upasuaji, hukutwa tumboni mna kilogramu nne hadi tano za taka za plastiki. Kwa mfugaji asiye na uwezo wa kutibu mifugo yake, mifugo hiyo hufa kutokana na kula au kumeza plastiki."

**KAULI YA NEMC**

Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Morogoro-Rufiji, Abel Sembeka anasema Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inakataza uchafuzi wa mazingira wa aina yoyote.

Anasema kifungu cha 118(1) cha sheria hiyo kinaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga vituo vya kuweka taka kwa muda ambavyo vitatumika kukusanyia taka ngumu kwenye majiji, manispaa, miji au maeneo mengine ambayo kiwango kikubwa cha taka ngumu huzalishwa.

Sembeka anasema sheria inaelekeza jukumu la kusimamia taka ni la miji, halmashauri na manispaa kwa kuwa ndiyo wenye maeneo zinakozalishwa taka hizo, pia wanawatambua watu wao vizuri.

"Kazi yetu (NEMC) kwenye hili la taka, pale tunapoona kuwa kuna shida na wananchi wanalalamika, huwa tunaiandikia barua halmashauri husika ili ichukue hatua haraka za kuweka mazingira kwenye hali ya usalama ili kuepuka athari," anasema.

Sembeka anakiri kuwa na taarifa za tatizo la mrundikano wa taka za plastiki katika Manispaa ya Morogoro, akilitaja ndiyo sababu ya manispaa hiyo kushika nafasi ya mwisho kitaifa kwa miaka ya hivi karibuni kwenye utunzaji mazingira.

Manispaa ya Morogoro si eneo pekee linalokabiliwa na kukithiri kwa taka za plastiki. Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) ya mwaka 2022 inaonesha zaidi ya tani milioni 400 za plastiki huzalishwa kila mwaka kote duniani.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa kati yake, chini ya asilimia 10 huchakatwa ili kutumika tena, huku kila mwaka zaidi ya tani milioni 19 hadi milioni 23 za plastiki huingia katika mito, maziwa na bahari.

**ITAENDELEA KESHO**

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza kuanza kuingia kwa viongozi wakuu wa Nchi za Afrika, kushiriki mkutano wa Nishati, unaotarajiwa kuanza leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MKUTANO WA NISHATI

## Ikulu: Watumishi wafanyie kazi nyumbani

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka ameagiza watumishi wa umma katika mkoa wa Dar es Salaam kufanyia kazi nyumbani isipokuwa wale ambao mazingira yao ya kazi yanawataka kuwapo vituoni leo na kesho kutokana na barabara tisa kufungwa kupisha Mkutano wa Nishati wa 'Mission 300'.

Amesema wafanyakazi ambao wanalazimika kuwapo kazini ni wa vyombo vya usalama, sekta ya afya na sekta ya usafiri na usafirishaji.

Vilevile, alisema benki hazitafungwa na biashara katika Soko la Kariakoo zitaendelea kufanyika na kwamba hoteli na migahawa nayo haitafungwa.

Balozi Kusiluka alisema katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari kuwa waajiri katika sekta binafsi wanashauriwa kutoa rukhsa kwa watumishi wao katika mkoa wa Dar es Salaam kufanyia kazi nyumbani au kuweka utaratibu ambao hautasababisha changamoto ya usafiri kutokana na kufungwa kwa barabara hizo. Mkutano huo umeandaliwa kati ya serikali, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ukihudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan; Marais wa Nchi za Afrika 24; wawakilishi wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika 21; Wakuu wa Taasisi za Kimataifa sita wakiwemo Rais wa WB, Rais wa Benki ya Dunia (WB), Ajay Banga, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina, na Rais wa Taasisi ya Rockefeller.

Washirika wa maendeleo watano watashiriki mkutano huo, na washiriki wengine 2,600 wa ndani na nje ya Tanzania ambao wamejisajili kwa ajili ya mkutano huo.

Miongoni mwa shughuli zitakazofanyika katika mkutano huo ni pamoja na kutia saini Mpango Mahususi wa Nishati wa Afrika (awamu ya kwanza) utakaozishirikisha nchi 14 za Tanzania, Malawi, Chad, Nigeria, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Niger, Liberia, Msumbiji, Madagascar, Zambia, Mali, Ivory Coast na Mauritania.

Washiriki wa mkutano huo pia watajadili namna ya kutumia fursa ya ushawishi kwa wadau wa maendeleo kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya nishati jadidifu ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, alisema jana kuwa baada ya mkutano huo, Rais Samia anatarajia kuwa na mazungumzo na wakuu hao wa nchi kuhusu masuala ya ushirikiano na nafasi ya Tanzania katika kushirikiana na nchi hizo.

Alitaja nchi ambazo wakuu wa nchi wanashiriki katika mkutano huo kuwa ni Algeria, Visiwa vya Comoro, Malawi, Zambia, Sierra Leone, Liberia, Somalia, Lesotho, Botswana, Guinea Bissau, Kenya, Burundi, Mauritania, Congo Brazzaville, Madagascar, DRC, Libya, Khartoum Sudan, Ethiopia, Nigeria, Ghana, Djibout, Togo na Gabon.

Viongozi wengine wanaohudhuria ni Makamu wa Rais wa Gambia, Makamu wa Rais wa Benin, Waziri Mkuu wa Ivory Coast, Waziri Mkuu wa Uganda, Waziri Mkuu wa Visiwa vya Sao Thomé, Waziri Mkuu wa Equatorial Guinea, Naibu Waziri Mkuu wa Ufalme wa Eswatini na Naibu Waziri Mkuu wa Namibia.

Juzi Jeshi la Polisi lilitangaza kufunga kwa muda barabara tisa zinazoelekea katikati ya jiji ili kupisha msafara wa viongozi.

Jeshi hilo lilisema kuwa kutokana na sababu za kiusalama, wanaotumia pikipiki na bajaji hawataruhusiwa kuingia katikati ya jiji.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Kikwete aonya wanaotumia kivuli cha dini kujenga chuki

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete amewaonya watanzania kuacha kutumia mwamvuli wa dini kujenga chuki na kuleta mifarakano katika jami, hali inayochochea machafuko na uvunjifu wa amani.

Kikwete ambaye ni mwasisi wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT), alisema hayo mjini Morogoro mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kamati, akiwaasa viongozi wa dini kusimama imara kuhakikisha Tanzania inaendelea kubaki kuwa kisiwa cha amani, utulivu na umoja.

Alisema amani na utulivu kamwe haviwezi kununuliwa dukani badala yake ni lazima watanzania waendelee kuimarisha undugu na mshikamano na kuepuka kubaguana kwa misingi yoyote, ikiwamo ya kiimani, rangi na kabila.

Alitolea mfano chachu ya kushauri uanzishaji taasisi hiyo enzi za serikali aliyoongoza kuwa kulisababishwa na mgogoro wa kidini ulioibuka wa kuchinja kati ya waumini wa Kiislam na Kikristo ambapo licha ya kuanzia eneo dogo la Katoro, watu waliusambaza na kuuchochea kuwa wa kiimani na kuleta machafuko, mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali.

"Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania) tukaitisha mkutano mkubwa sana kuwahi kutokea kwa kuwashiriaha viongozi wa dini zote, wakala na kulala pamoja ili kila mmoja amzoee mwenzake na ukawa mwanzo wa kuanzisha chombo hiki," alisema Rais mstaafu huyo.

Sheikh Alhad pia aliwahimiza viongozi wa dini kufanya matendo mema kwa kuwa wao wanafananishwa na chumvi ambayo ni kiungo muhimu katika mboga. Ikichafuka, haiwezi kusafishwa na kitu chochote.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima alisema mkoa huo miaka ya zamani ulikuwa unasifika kwa migogoro ya ardhi na wakulima na wafugaji. Tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, sifa hiyo inatoweka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini JMAT, Azim Dewji alisema jukumu la kulinda amani ni la kila mmoja na hata vyama vya siasa ni vyema vikalinda hilo na kufanya siasa ya staha kwa sababu Tanzania ni ya wananchi wote.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MTWARA, LINDI NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MADABA, NAMTUMBO NA TUNDURU.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumanne tarehe 28 Januari hadi siku Jumatatu tarehe 03 Februari, 2025
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.


***KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa leo tarehe 20 Januari, 2024 na:**


**Christina P. Ballali**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

TANGAZO

# TANZANIA REVENUE AUTHORITY



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya Rinan Mining Investment Tanzania Limited ya Mkoa wa Songwe wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa Walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imefanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo Said Salim Bakhresa aliyeshinda nafasi ya kwanza ya kuwa Mlipakodi Binafsi mwenye hadhi ya Juu (High Net Worth Individual) wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa Walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliyofanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo mlipakodi mdogo wa Kariakoo Bw. Faisal Abdulsatar wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa Walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imefanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo mwakilishi wa Kampuni ya Glitter Gems Limited ya Mkoa wa Manyara wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa Walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imefanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo Mlipakodi mdogo wa Mkoa wa Mtwara, Bw. Jumbe Bakari wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa Walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imefanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo Mtendaji Mkuu wa benki ya NMB Bi. Ruth Zaipuna kwa kuibuka mshindi wa jumla wa ulipaji kodi kwa hiari kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Tuzo hiyo alikabidhiwa wakati wa hafla ya kuwashukuru na kuwapa tuzo walipakodi bora wa mwaka 2023/2024 iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

# TANGAZO




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo aliyopewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuwa mhamasishaji namba 1 wa ulipaji kodi. Tuzo hiyo ilikabidhiwa kwake na Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TRA Mussa Uledi pamoja na Kamishna MKuu wa TRA Yusuph Juma Mwenda wakati wa hafla ya kuwashukuru na kuwapa tuzo walipakodi bora wa mwaka 2023/2024 iliyofanyika jijini Dar es Salaam.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akikabidhi tuzo kwa Kampuni ya Tanzania Breweries Public Limited Company kwa kuibuka mshindi wa pili katika kipengele cha walipakodi kwa hiari zaidi wa kampuni na wenye kiasi kikubwa cha mchango wa mapato wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliyofanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CRDB PLC Abdulmajid Nsekela kuibuka mshindi wa tatu katika kipengele cha walipakodi kwa hiari zaidi wa kampuni na wenye kiasi kikubwa cha mchango wa mapato wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 ambayo imefanyika tarehe 23 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bw. Yusuph Juma Mwenda (kulia) akikabidhi tuzo kwa Kampuni ya Airtel Tanzania Public Limited Company wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliyofanyika tarehe 23 januari, 2025 jijini dar es salaam.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kutoa uraia kwa wachezaji kupitia klabu ni kufungua mlango mgumu kuufunga

**WIKI** hii, Idara ya Uhamiaji, ilithibitisha kuwapa uraia wachezaji watatu wa Singida Black Stars, Emmanuel Kwame Keyekeh, Josephat Arthur Bada na Mohamed Damaro.

Taarifa kutoka kwa Msemaji, Mkuu wa Idara ya Uhamiaji, Paul Mselle, ilithibitisha wachezaji hao kupatiwa uraia wa Tanzania.

Taarifa ilisema wachezaji waliomba na walipewa kwa mujibu wa vifungu vya 9, 23 vya Sheria ya Uhamiaji, sura ya 357. Na kwamba wamepewa uraia wa Tanzania kwa Tajnisi.

Hata hivyo, utoaji huo wa uraia ulizua mjadala mkubwa, si kwa wapenzi, wadau na mashabiki wa soka pekee, bali hata kwa raia wa kawaida na watu wa kada zingine, wakiwamo wanasheria.

Wengi walidhani kuwa wachezaji hao, Keyekeh raia wa Ghana, Bada wa Ivoct Coast na Damaro, akitokea Guinea, bado hawakuwa na vigezo vinavyowawezesha kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, hatupo hapa kubishana na mamlaka kwa sababu yenyewe ndiyo yenye uamuzi wa mwisho wa kutoa uraia kutokana na vigezo vyao wanavyoona vinakidhi sheria. Lakini kama imetoa kwa sababu za kimpira ili walisaidie taifa kama ambavyo inatajwa, basi kutakuwa na maswali ya kujiuliza.

Kwanza, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Morocco, amewahitaji wachezaji hawa ili baadaye awajumuishe kwenye kikosi hicho baada ya kujiridhisha kuwa na vipaji maalum?

Kama si hivyo, kocha Morocco alisiporidhika nao na kutowaita kwenye kikosi cha timu ya taifa? Tuna uhakika mpaka kufikia CHAN na AFCON, wachezaji hawa watakuwa kwenye kiwango kichachotakiwa cha kuichezea Stars?

Tunaamini kama wamepewa kwa sababu ya 'uspesho' wao kwenye soka na kuwa watalisaidia taifa, lakini sheria ya FIFA zinapinga hilo, hivyo hawatocheza CHAN wala AFCON, ndiyo maana tunaona kuna shida sehemu.

Tunasema si rahisi kucheza kwa sababu kwa mujibu wa sheria za FIFA ni kwanba. Mchezaji aliyebadili uraia ili kuichezea nchi husika, anapaswa kuishi kwenye nchi yake mpya kwa miaka isyopungua mitano ili apate sifa ya kuichezea timu ya taifa, sifa ambayo wachezaji hao wanaikosa.

Lakini pia mchezaji anapaswa kuwa amesafiri kwenye nchi yake hiyo mpya akiwa na umri wa miaka 10 na 18, huku FIFA wakihitaji ushahidi wa tiketi, visa, vibali vya ukazi vyenye tarehe sahihi.

Tatu, FIFA watachunguza kama sababu ya kubadili uraia mchezaji haikuwa ya kimpira, yaani wakigundua alibadili ili achezee timu ya taifa, hawatoi ruhusa hiyo. Kwa vigezo hivyo vyote tuna wasiwasi kama wanaweza kuwa navyo, hivyo watakuwa wamepewa tu kama zawadi, huku wakipata bahati ya mtende ya kutokidhi vigezo vingi, zaidi ya uamuzi wa mwisho wa mamlaka.

Hapa ndipo linapokuja swali lingine. Je suala hili kweli limefanywa kwa ajili ya manufaa ya timu ya taifa, au klabu ya Singida Black Stars? Kwa nini wachezaji walioomba uraia wawe kutoka klabu moja tu?


Tunaona kama hili litakuwa limefungua mlango kwa klabu nyingi za Tanzania kuwashawishi wachezaji wao kuomba uraia kwa kutumia vigezo kama ambavyo vimetolewa kwa hao waliopewa.

Tayari wachezaji tisa wa Simba wameomba wapewe uraia kwa sababu hizo hizo ambazo wa Singida Black Stars wamesababisha wapewe. Klabu ya Simba imethibitisha hilo, ikiwa nyuma ya wachezaji wake kutaka wapatiwe uraia kama walivyopewa wenzao.

Huu ni mtego ambao umeingiwa. Vyovyote itakavyokuwa, kama ikikubali, basi nchi hii itakuwa na raia wengi ambao ni wachezaji, kazi yao kubwa ikiwa ni mpira, kazi ya muda mfupi, wakistaafu wanajazana hapa hapa. Pili klabu zitakuwa zinatumia njia hii kukwepa kulipa vibali vya kazi na kuishi nchini, hivyo itakuwa ni hasara tu kwa taifa ambalo lilikuwa liingize mapato yake kupitia sekta hiyo ya michezo.

Tatu kwa utaratibu huo wa kutoa uraia kwa wachezaji kupitia klabu, zinaweza kufanya hivyo kila msimu wa usajili kwa wale waliopewa wanaposhuka viwango, hivyo tunaona mamlaka husika imefungua mlango ambao unaweza kuwa mgumu kuufunga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# TFF iongeze idadi ya wachezaji wa kigeni kuepuka sakata la uraia

Na Adam Fungamwango

**SAKATA** la kupewa uraia kwa wachezaji wa Singida Black Stars, Emmanuel Kwame Keyekeh, Josephat Arthur Bada na Mohamed Damaro, ndiyo limekuwa gumzo wiki hii nchini.

Keyekeh raia wa Ghana, Bada wa Ivoct Coast na Damaro, akitokea Guinea, kwa sasa ni raia wa Tanzania baada ya wao wenyewe kuomba kwa mujibu wa Idara ya Uhamiaji.

Taarifa ilisema walipewa kwa mujibu wa vifungu vya 9, 23 vya Sheria ya Uhamiaji, sura ya 357, wakitajwa kuwa ni raia wa Tanzania kwa Tajnisi.

Kupewa uraia kwa wachezaji hao kumeibua hisia kutoka kwa wanamichezo, raia wa kawaida na wanasheria kila mmoja akiongea lake, lakini baadhi wakiamini hawakupaswa kupewa kutokana na kutokidhi vigezo vingi vilivyowekwa kwa uombaji.

Baadhi wakaenda mbali na kusema hata ule 'uspesho' wa wachezaji hao kwa ajili ya kuichezea timu ya taifa, hawauoni, kwani pamoja na kwamba ni wazuri, lakini si bora kiasi cha kulazimika kuwapa uraia kwa mtindo huo.

Pamoja na hayo, sheria za Shirikisho la Mpira wa Miguu (FIFA), ukizisoma haziwapi wachezaji hao nafasi ya kuichezea Timu ya Taifa, Taifa Stars.

Zinasema hivi. Mchezaji aliyebadili uraia anapaswa kuishi kwenye nchi yake mpya kwa miaka isiyopungua mitano ili apate sifa ya kuichezea timu ya taifa. Sidhani kama wanayo.

Mchezaji anapaswa kuwa amesafiri kwenye nchi yake hiyo mpya akiwa na umri wa miaka 10 na 18, huku FIFA wakihitaji ushahidi wa tiketi, visa, vibali vya ukazi vyenye na tarehe sahihi.

Tatu, FIFA watachunguza kama sababu ya kubadili uraia mchezaji haikuwa ya kimpira, yaani wakigundia alibadili ili acheze timu ya taifa, hawatoi ruhusa hiyo.

Kwa maana hiyo, wachezaji hao raia wa Tanzania wataendelea kuitumikia Singida Black Stars kwenye mechi zake za Ligi Kuu.

Inawezekana wachezaji wameomba ili kuipunguzia mzigo wa vibali vya kuishi na kufanya kazi katika klabu yao.

Au pia wameomba kwa kukubaliana na klabu kutokana na kuzidisha idadi ya wachezaji 12 wa kigeni iliyowekwa kikanuni. Kwa maana hiyo Singida itakuwa na wachezaji 12 wa kigeni, na hao watatu hivyo ingekuwa na wachezaji 15 ambao hawajazaliwa nchini.

Mimi nadhani imefika wakati Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kuongeza wachezaji wa kigeni msimu ujao kutoka 12, angalau kuwa 15.

Nadhani wakati wa kutoa maoni ya idadi ya wachezaji wa kigeni, kamati zifikirie namna gani ya kuongeza zaidi kuliko kupunguza.

Wadau wengi wa soka nchini wanabainisha kuwa vipaji vya wachezaji nchini vimezidi kupungua, na hata wachezaji wa Kitanzania ambao wana vipaji, mara nyingi havina mwendelezo kutokana na mambo mbalimbali, ikiwamo nidhamu ya kuishi kwa wanamichezo, hivyo wengi hata timu zinazoitwa au kujiita ndogo, nazo zimeamua kusajili kutoka nje ya nchi.

Nafikiri kuongezwa kwa idadi ya wachezaji kutawafanya wachezaji wanaozaliwa Tanzania kuanza kujitafakari upya, kujitambua, kupigania namba, kujitunza, lakini pia kutazifanya mamlaka kutolazimika kutoka uraia kwa Tajnisi, kirahisi hivyo.

Nafikiri pia, hakuna wachezaji wengi wa nje watakaoomba, kwani nadhani ufinyu wa idadi ya wageni wanaoruhusiwa kwa klabu moja ndiyo sababu ya yote haya na si vinginevyo.

## TANGAZO

# FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing
Homes within your reach

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Dec. 2024 | Robo Mwaka iliyopita 30th Sep. 2024 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 5,218 | 2,571 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,601,250 | 3,656,967 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,739,465 | 3,287,276 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 35,266,802 | 33,983,904 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,217,111 | 1,107,515 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,767,980 | 1,767,980 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 167,851 | 197,088 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **43,765,677** | **44,003,301** |
| | | | |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 2,322,479 | 2,461,997 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 254,370 | 437,686 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 603,662 | 544,848 |
| 27 | Dhima Nyingine | 287,187 | 232,444 |
| 28 | Madeni | 20,993,595 | 21,229,109 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **24,461,294** | **24,906,084** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **19,304,384** | **19,097,217** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,383,974) | (3,454,708) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 451,134 | 242,478 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 341,393 | 413,616 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **19,304,384** | **19,097,217** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 1,314,544 | 1,288,186 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 375,205 | 426,384 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 44.11% | 43.40% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.67% | 3.73% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1473.30% | 1325.34% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 80.58% | 77.23% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89.37% | 86.18% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -5.67% | 3.02% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.54% | 7.74% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2024 | 31st Dec. 2023 | 31st Dec. 2024 | 31st Dec. 2023 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,612,479 | 1,485,112 | 5,838,376 | 4,833,462 |
| 2 | Gharama za Riba | (671,689) | (460,199) | (2,191,848) | (1,487,940) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **940,790** | **1,024,913** | **3,646,528** | **3,345,522** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 43,710 | 26,368 | (115,956) | (106,888) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **90,504** | **(87,041)** | **499,431** | **205,398** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (14,950) | (2,582) | (14,618) | (1,237) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 78,542 | (92,791) | 416,569 | 152,147 |
| | 6.3 Gawio | - | - | 40,100 | 36,900 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 26,912 | 8,332 | 57,380 | 17,588 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(827,441)** | **(785,735)** | **(3,499,256)** | **(3,040,590)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (418,568) | (584,397) | (1,892,860) | (1,774,369) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (408,873) | (201,338) | (1,606,396) | (1,266,221) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **247,562** | **178,505** | **530,747** | **403,442** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (38,906) | (33,378) | (79,614) | (51,397) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **208,656** | **145,127** | **451,134** | **352,045** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **208,656** | **145,127** | **451,134** | **352,045** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 26 | 27 | 26 | 27 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.96 | 0.67 | 2.07 | 1.61 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.48% | 0.40% | 1.03% | 1.00% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.09% | 0.77% | 2.35% | 1.88% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 80.23% | 83.78% | 84.40% | 85.63% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.44% | 3.19% | 2.44% | 10.17% |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Jina na Cheo : | Saini | | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Amulike E. Kamwela **(Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | ............................. | 24.01.2025 |
| Antidius Kabyemela **(Kaimu Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | ............................. | 24.01.2025 |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | ............................. | 24.01.2025 |

### KEY FINANCIAL HIGHLIGHTS

| PROFIT BEFORE TAX | REVENUE GROWTH | MORTGAGE BOOK |
|---|---|---|
| 32% YOY | 17% YOY | 4% QOQ |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.12.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.10.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,213,719)** | **413,616** | **-** | **95,831** | **19,095,728** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 208,656 | - | - | - | 208,656 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | 72,223 | (72,223) | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(2,932,840)** | **341,393** | **-** | **95,831** | **19,304,384** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (30.09.2024)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.07.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,131,168)** | **232,247** | **-** | **95,831** | **18,996,910** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 98,818 | - | - | - | 98,818 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (181,369) | 181,369 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (30.09.2024)** | **21,800,000** | **-** | **(3,212,231)** | **413,616** | **-** | **95,831** | **19,095,728** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2024

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Dec. 2024 | 30th Sept. 2024 | 31st Dec. 2024 | 31st Dec. 2023 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **247,562** | **116,004** | **530,747** | **403,442** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | (18,994) | 71,507 | 206,725 | (595,372) |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,238,096) | (2,714,165) | (8,086,190) | (8,107,900) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (139,518) | 72,286 | 441,874 | 968,818 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (108,665) | (49,848) | 336,642 | (366,748) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (53,504) | (8,578) | (345,885) | (84,859) |
| | - Kodi iliyolipwa | (38,906) | (17,186) | (79,614) | (51,397) |
| | - Mengineyo | 6,013 | 29,577 | 58,233 | 57,969 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(1,344,108)*** | ***(2,500,403)*** | ***(6,937,467)*** | ***(7,776,047)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | 40,100 | 36,900 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | 26,951 | 30,759 | (28,723) | 917,695 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 55,717 | (57,525) | (688) | 801 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***82,668*** | ***(26,766)*** | ***10,689*** | ***955,396*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu kwenda CRDB | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | (235,513) | 3,022,737 | 4,784,872 | 4,204,994 |
| | Mengineyo (bainisha) | (54,587) | (53,100) | (106,200) | (100,890) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(290,100)*** | ***2,969,637*** | ***4,678,672*** | ***4,104,104*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **(1,551,540)** | **442,468** | **(2,248,106)** | **(2,716,547)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | 3,289,847 | 2,847,379 | 3,986,413 | 6,696,939 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 6,376 | 0 | 6,376 | 6,021 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **1,744,683** | **3,289,847** | **1,744,683** | **3,986,413** |

### TARRIF

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 18% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Restructuring/Rescheduling Fee | 1% of the restructured/ rescheduling amount |
| 7 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 8 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 9 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid from Bank or Financial Institution |
| 10 | Annual Review Fee | NIL |
| 11 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 12 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Charles Mugila **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | ............................. | 24.01.2025 |
| Margaret Ikongo **Mkurugenzi** | (Imesainiwa) | ............................. | 24.01.2025 |

# Nyuki wavamia shuleni na kujeruhi wanafunzi, walimu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

WANAFUNZI 27 na walimu wawili wa Shule ya Msingi Sayuni, wilayani Manyoni, mkoa wa Singida wamejeruhiwa na kulazwa hospitalini baada ya kundi la nyuki kuwavamia na kuwashambulia. Mwalimu wa shule hiyo, Neema Ng'aa, akizungumza juzi baada ya Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk.Vicent Mashinji kutembelea shule hiyo, alisema tukio hilo lilitokea juzi wakati wanafunzi hao wakiwa darasani.

"Nyuki walipovamia shuleni, wanafunzi walianza kukimbia ovyo kujiokoa na walimu waliokwenda kuwasaidia wanafunzi, nao walishambuliwa na kujeruhiwa," alisema.

Mwalimu Bless Mwarabu alisema kuwa baada ya nyuki kuvamia shuleni, ilipigwa kengele, hali iliyosababisha nyuki kuongeza kasi ya kushambulia wanafunzi na kuwajeruhi. Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni, Dk. Lucy Deo, alisema kuwa baada ya kupata taarifa za tukio hilo, walipeleka magari matatu ya kubeba wagonjwa (ambulance) kwa ajili ya kuwachukua majeruhi na kuwafikisha hospitalini kwa ajili ya matibabu.

**"Majeruhi tuliowachukua ni 27 ambao ni wanafunzi na walimu wawili, tuliwapa matibabu na baadhi yao waliruhusiwa na wengine bado wanaendelea na matibabu," alisema.**

"Majeruhi tuliowachukua ni 27 ambao ni wanafunzi na walimu wawili, tuliwapa matibabu na baadhi yao waliruhusiwa na wengine bado wanaendelea na matibabu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Mashinji, ambaye alifika katika shule hiyo, alielekeza watendaji wote sehemu zinazotoa huduma kwa jamii, wadudu na wanyama hatarishi wadhibitiwe.

"Nielekeze shule zote nikikuta nyuki shuleni, mimi ninaanza na mwalimu wa mazingira na baadaye mwalimu mkuu, maana nyuki kuweka makazi yao shuleni wakati hawasomi wala hakuna kozi ya nyuki, kuna haja gani ya kuwa nao mazingira ya shule," alionya.

Makundi ya nyuki yamekuwa yakiweka makazi kwenye madarasa ya shule na nyumba za ibada mkoani Singida na kusababisha wananchi kushambuliwa.




## KUJIUNGA NA KOZI YA
## WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Kituo cha Mafunzo cha ATCL kinafuraha kutangaza ufunguzi wa maombi ya kozi yake ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew). Kozi hii ya miezi mitatu (3) imepangwa kuanza tarehe 17 Machi, 2025.

**Sifa za mwombaji**

**Umri:** Kuanzia miaka 18 hadi miaka 25.

**Michoro mwilini:** Muombaji asiwe na michoro ya kudumu mwilini (tattoos).

**Muonekano:** Awe mwenye akili timamu na mwenye urefu wa kuanzia futi 5"4 (162cm).

**Elimu:** Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu angalau wa masomo manne kwa alama "D". Somo la Kiingereza na Jiografia ni lazima.

**Lugha:** Awe na uwezo wa kuongea na kuandika kwa ufasaha Kiswahili na Kingereza. Aidha, muombaji mwenye uelewa wa lugha zingine zaidi za kigeni kama Kiarabu, Kichina au Kifaransa atapewa kipaumbele.

**Uraia:** Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kusoma nchini. Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kuwasilisha matokeo ya vyeti vyao Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) ili kupata ulinganifu wa matokeo.

**Barua ya maombi**

**Maombi yote ni lazima yaambatanishwe na nyaraka zifuatazo:** Nakala ya cheti cha kidato cha nne na vyeti vingine vya shule/chuo alichohitimu. Nakala ya cheti cha kuzaliwa. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonesha umbo lote ukubwa wa 6x8. Wasifu wa muombaji (Curriculum Vitae – CV).

Kuwasilisha Maombi Maombi yawasilishwe kwa Mkuu wa Chuo, Jengo la Chuo cha ATCL (Ofisi ya Utawala), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Terminal One au kupitia barua pepe: **training@airtanzania.co.tz.** Maombi yote yatumwe kabla ya tarehe 13 Februari 2025.

Anuani
Mkuu wa Chuo,
ATCL Training Center,
S.L.P 543, Dar Es Salaam.





Prof Mohamed Janabi

# China yakabidhi Muhimbili vifaatiba vya Sh. bilioni 125/-

**Na Christina Mwakangale**

CHINA imekabidhi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) vifaatiba mbalimbali vyenye thamani ya Sh. bilioni 125, vikiwamo kwa ajili ya kukuza uoni wa mishipa ya damu na fahamu wakati wa upasuaji.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alikabidhi vifaa hivyo kwa Waziri wa Afya, Jenista Mhagama hospitalini huko mwishoni mwa wiki kwa niaba ya Serikali ya Watu wa China.

Waziri Jenista, akizungumza baada ya kupokea msaada huo, alisema ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya ushirikiano kati ya Tanzania na China kwenye sekta ya afya.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia MNH kuboresha huduma za afya na kukabiliana na changamoto mbalimbali katika utoaji huduma za afya bora kwa wananchi.

"Ushirikiano kati ya nchi hizi mbili utaendelea kuwa na manufaa zaidi kwa pande zote, ikiwamo kuleta wataalam wa afya mabingwa wabobezi na vifaa vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu ili kuongeza ubora wa huduma.

"Ninapongeza uongozi wa MNH, kwa kuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji ushirikiano huu. msaada huu utachangia katika kuboresha utoaji huduma za afya na kutoa matokeo chanya kwa wananchi," alisema Jenista.

Balozi wa China nchini, Mingjian, alishukuru Wizara ya Afya, MNH pamoja na timu ya madaktari kutoka China waliomo nchini, kwa michango yao muhimu katika ushirikiano wa muda mrefu kati ya nchi hizo mbili kwenye sekta ya afya.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi alishukuru China kwa msaada huo na kuomba ushirikiano zaidi katika maendeleo ya rasilimali watu na teknolojia za kisasa.

"Ushirikiano huu ni fursa kwa madaktari wetu kupata mafunzo ya ubingwa nchini China yatakayoboresha ujuzi wao na kuwafundisha teknolojia na mbinu za kisasa, hasa kwenye AI (akili mnemba) zinazohitajika katika huduma za afya," alisisitiza Prof. Janabi.

Alisema miongoni mwa vifaa vilivyokabidhiwa vitasaidia daktari awapo chumba cha upasuaji kuona kwa ukubwa mishipa midogo ya damu na fahamu kwa kutumia kifaa maalum chenye darubini ambacho huvaliwa kama miwani.

# Jafo atoa maagizo matano akizindua bodi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk.Selemani Jafo, ameagiza Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), kuleta mabadiliko katika uzalishaji na udhibiti wa zana za kilimo zinazoingia kutoka nje ya nchi, ikiwemo kutopata hati chafu na matumizi sahihi ya fedha.

Dk. Jafo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki Jijini Arusha, alipokwenda kuzindua Bodi ya Wakurugenzi ya CAMARTEC.

Alisisitiza bodi hiyo kusimamia vizuri kazi za kituo hicho, ikiwemo kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuhakikisha zana za kilimo zinawafikia wananchi wakiwemo wakulima katika matumizi sahihi ya zana za kilimo.

Alisema lazima bodi hiyo kuendelea kutoa ushauri pamoja na kusimamia menejimenti na watumishi wake, ili kuhakikisha wanaleta tija katika kituo hicho na kuhakikisha wanatoa matunda bora.

"Lazima muwe wabunifu wenye upendo na nidhamu kazini na kujifunza zaidi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia, lazima bodi hii muwe wakali katika kusimamia kazi ili Camartec ibadilike na katika uzalishaji wa zana za kilimo, kwani kilimo ni tija na endapo tukifanya vizuri tutaisaidia Wizara ya Kilimo katika masuala ya ubunifu,"alisema.

Alisema ni muhimu bodi hiyo kuleta mabadiliko zaidi katika ufanisi ili kuleta tija na mabadiliko makubwa zaidi ingawa alikiri upungufu wa watumishi zaidi ya 72 katika idara mbalimbali lakini watumishi waliokuwepo ofisini wahakikishe wanajiuliza wanazalisha nini.

"Nahitaji mabadiliko katika bodi hii kwani tangu mwaka 1982 hadi leo hii CAMARTEC imefanya nini katika ubunifu, lakini pia menejimenti saidieni bodi kuhakikisha taasisi hii inaenda mbele zaidi ikiwemo matumizi ya usimamizi wa rasilimali haswa katika matumizi ya fedha,"alisema.

Alisisitiza bodi kuhakikisha kiwanda hicho hakipati hati chafu pamoja na mkaguzi wa ndani kufanya kazi zaidi ili kuzuia upatikanaji wa hati chafu.

Pia aliagiza taasisi zote za wizara hiyo kutenga bajeti kwa ajili ya kitengo cha habari na mawasiliano ikiwemo vyombo bora vya usafiri ili iwe rahisi kwenda kwenye miradi ya ukaguzi.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Needpeace Wambuya akimwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, alisema anaamini bodi hiyo itasimamia kwa ukamilifu utafiti na majaribio ya teknolojia, kwa ajili ya zana za kilimo zinazoingizwa nchini kutoka nje ya nchini.

"Bodi hii, tunaamini itafanya kazi nzuri ikiwemo kuhakiki kwa ukaribu zana za kilimo zinazoingizwa nchini kutoka nje ya nchini,"alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CAMARTEC, Godfrey Mwinama, alisema kituo hicho kimefanikiwa kuunda zana mpya 42 zinazozalisha zana mbalimbali kwa ajili ya kuongeza tija katika kilimo.

Alisema pia wana changamoto ya uhaba wa wafanyakazi, kukosekana kwa karakana ikiwemo ukosefu wa maabara, hivyo CAMARTEC inajenga viwanda darasa ili kuwezesha Watanzania kupata zana za kilimo kwa ukaribu.

Mwenyekiti wa Bodi ya CAMARTEC, Prof. Valerian Silayo, akizungumza baada ya kuanza kutumikia wadhifa huo, alisisitiza juu ya kuunganisha uzoefu wao wa utendaji kazi katika kuhakikisha kituo hicho kinafikia malengo yaliyokusudiwa ikiwemo kusaidiwa upatikanaji wa fedha za kuendesha kituo hicho kwa wakati.

# Mawaziri wa nishati EAC kujadili uzalishaji umeme

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAWAZIRI kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na watumiaji wakubwa wa nishati wanatarajia kukutana mkoani Arusha katika Mkutano wa Ushirikiano wa Nishati wa Afrika Mashariki (EA-ECS), kuanzia Januari 29-30.

Mkutano huo utajikita kufungua fursa kwa sekta binafsi, kuhimiza kuwepo kwa mseto wa nishati pamoja na uzalishaji wa umeme kwa matumizi ya kibiashara na biashara za viwandani.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu (Sekta ya Miundombinu, Uzalishaji, Jamii na Siasa), Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Andrea Malueth, alisema kwa kuzingatia mafanikio ya mwaka jana, mkutano huo utakuza ushirikiano Afrika Mashariki.

Alisema kuwa mkutano huo pia utaangazia dira ya EAC ya ushirikiano wa kina wa kikanda na jukumu muhimu la kukuza viwanda na ushirikiano miongoni mwa wadau.

> **"Kiini cha ukuaji huu wa kikanda wa shughuli za uwekezaji ni Sekretarieti ya Afrika Mashariki ambayo inawakutanisha wawekezaji na watengeneza sera pamoja na EnergyNet, kujikita katika**

Alisema mkutano huo utawakutanisha wazalishaji nishati binafsi kutoka Afrika na wadau wa uhandisi, ununuzi, ujenzi, na fedha ambao watatathmini uwezekano wa uwekezaji na uvumbuzi ulioanzishwa na kampunimuhimu kimkakati, ikijumuisha vituo vya data vya Afrika na iXAfrica.

"Kiini cha ukuaji huu wa kikanda wa shughuli za uwekezaji ni Sekretarieti ya Afrika Mashariki ambayo inawakutanisha wawekezaji na watengeneza sera pamoja na EnergyNet, kujikita katika "utajiri wa rasilimali. Upatikanaji wa nishati. Fursa za uwekezaji." Alisema.

Alisema EA-ECS itakaribisha wanasiasa na viongozi mashuhuri kutoka nchi zote za Afrika Mashariki na sekta zake za nishati katika mkutano huo ambapo wataungana na wakuzaji biashara wa sekta binafsi.

Mtayarishaji wa EnergNet, Elisa Palmioli alisema: "Miaka 10 kutoka sasa, tabaka la kati la watu wa Afrika Mashariki litakuwa na uthabiti zaidi wa kazi, fursa zaidi, na kipato zaidi ukilinganisha na hapo awali"

Alisema: "Reli mpya, viwanda, bandari na utalii vitalifanya eneo hili kuwa kivutio kikuu cha uwekezaji duniani na kujitwalia nafasi hiyo kutoka eneo la Asia na Amerika Kusini,"

Alitaja mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na njia kuu ya umeme ya Ethiopia-Kenya, jambo ambalo linasisitiza uwezekano wa mageuzi wa ushirikiano wa kuvuka mpaka kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mafanikio mengine ni watumiaji wa nje kuongeza hitaji la uzalishaji wa nishati ambapo mkutano huo utazingatia sekta ya madini na miundombinu ya kidijitali.



Askari polisi na viongozi wa Shirika la Kutetea Haki za Abiria (SHIKUHA), wakisikiliza kero za abiria katika kituo cha mabasi, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mazungumzo usafirishaji magadi soda yaanza rasmi

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha imekiri kuanza mazungumzo rasmi na Shirika la Reli Tanzania (TRC), kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya reli ya Kaskazini kutoka Arusha Mjini hadi Engaruka, Wilaya ya Monduli ili kurahisisha usafirishaji wa madini ya magadi soda yanayoanza kuzalishwa.

Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, alidokeza kuhusu mazungumzo hayo mwishoni mwa wiki, alipokutana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hashil Abdalah.

Waziri Jafo alikwenda Monduli, kuzindua ulipaji fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa wananchi 599 wanaomiliki maeneo ya ardhi katika vijiji vinne, vinavyopisha utekelezaji wa mradi wa kimkakati, uliokwama kwa zaidi ya miaka 20 wa kuzalisha madini hayo ya asili katika Bonde la Engaruka.

Diwani wa Engaruka, Onesmo Naikoyo, akizungumzia mradi huo, alisema wenyeji wana matarajio makubwa kwamba mradi huo utaimarisha miundombinu na kuinua hali yao ya maisha.

Alisema magadi soda ni malighafi inayotumika kuzalisha bidhaa nyingi duniani, ambapo kukamilika kwa mradi huo, kutatosheleza soko la ndani na mauzo ya nje ya nchi.

Aidha, magadi soda asilia katika uso wa dunia, hupatikana pia katika Ziwa Magadi lililoko nchini Kenya, Ziwa Natron nchini Tanzania na Uturuki.

Kwa mujibu wa ripoti ya kitaalamu, Mlima Oldonyo Lengai, ambao ni wa volcano hai uliopo jirani na Bonde la Engaruka, ndiyo unaozalisha magadi soda.

Inaelezwa kuwa, mlima huo ni chanzo cha magadi soda ambayo hutiririka na kuingia katika Ziwa Magadi, Natron, Balangida Gidalund, Balangida Lelu, Manyara na Ziwa Singida.



# Hospitali ya Rufani Bukoba yaanza upasuaji ubongo

**Na Titus Mwombeki,**
BUKOBA

MGANGA Mkuu wa Serikali, Dk.Grace Magembe amesema Hospitali ya Rufani Mkoa wa Kagera, Bukoba (BRRH), imeanza rasmi kufanya upasuaji wa awali wa ubongo kwa wagonjwa wa dharura.

Alitoa taarifa hiyo jana alipotembelea hospitali hiyo na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuwapunguzia wananchi wa Mkoa wa Kagera safari za kufuata huduma za namna hiyo katika Hospitali ya Rufani Kanda, Bugando ya mkoani Mwanza.

Alisema hatua hiyo imefanikishwa na kuwepo kwa vifaa vya kisasa ikiwemo mashine ya kisasa ya CT-Scan iliyowezesha madaktari kuanza kutoa huduma za upasuaji wa awali wa ubongo kwa wagonjwa wa dharura.

Katika ziara hiyo maalumu ambayo pia ililenga kukagua utoaji wa huduma za afya hospitalini hapo na kuona namna watumishi wanavyoendelea kuchukua tahadhari katika kujikinga na ugonjwa wa Marburg wakiwa kazini.

**Katika ziara hiyo maalumu ambayo pia ililenga kukagua utoaji wa huduma za afya hospitalini hapo na kuona namna watumishi wanavyoendelea kuchukua...**

"Nimefurahishwa sana kuona kuna mashine hii ilivyosaidia madaktari wetu kuwafanyia upasuaji wagonjwa hao hasa wale waliopata ajali na kuvuja damu kichwani. Kwa sasa wagonjwa hao wanapata huduma hapa kitu ambacho siyo cha kawaida kwa hospitali ya mkoa kutoa huduma hii, mara nyingi huduma kama hii hutolewa na hospitali za kanda au taifa," alisema Dk. Magembe.

Aidha, Dk. Magembe alitembelea pia jengo la dharura, kitengo cha kusafisha damu, kitengo cha watoto wachanga na kuwapongeza watumishi wa vitengo hivyo kwa kuendelea kutoa huduma bora, kujituma na kufuata miongozo ya kitaalamu ili kupunguza vifo vya watoto wachanga, wajawazito na kuokoa maisha ya Watanzania.

Dk. Magembe alisema serikali inaendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kusambaza vifaa tiba vya kisasa, kujenga hospitali mpya za wilaya na kuanzisha vituo vya afya ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Bukoba, Dk. Museleta Nyakiroto aliahidi kuendelea kusimamia ipasavyo utendaji kazi wa watumishi hospitalini hapo ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi kwa kufuata miongozo iliyotolewa na Wizara ya Afya.



Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (katikati mwenye kofia nyekundu), akikagua utekelezaji wa Mradi wa upanuzi wa Bandari ya Mwanza Kusini, jijini Mwanza mwishoni mwa wiki, inayotarajiwa kutumiwa na meli kubwa ya MV. Mwanza Hapa Kazi, itakapokamilika Mwezi Mei, mwaka huu. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Miradi tisa yasainiwa kumaliza kero ya maji Shinyanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MIRADI tisa ya maji yenye thamani ya Sh.bilioni 4.8 imesainiwa ili kumaliza tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama katika Halmashauri ya Shinyanga, Kishapu na Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Mkataba huo ulisainiwa kati ya Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na makandarasi mbalimbali, ikishuhudiwa na Mkuu waa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha.

Akizungumza wakati wa utiaji saini huo, Macha aliwaonya makandarasi wa miradi hiyo kutokuwa sehemu ya kundi la makandarasi wengine ambao wamekuwa wakifanya kazi zao bila ya kushirikisha wananchi katika maeneo inapotekelezwa miradi.

"Mkashirikishe wananchi wa maeneo husika pamoja na kuwapatia ajira zile ambazo wanauwezo nazo ili muwe na uhusiano mazuri," alisema Macha.

Aidha, aliuagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuwasilisha kwake taarifa ya ututekelezaji wa miradi hiyo kila ifikapo tarehe 15 ya kila mwezi ili kujua changamoto mapema ambazo zinawakabili makandarasi na kuzitatua.

Aliwasihi pia wananchi waitunze miundombonu ya miradi hiyo ya maji pamoja na kutumia maji ya kwenye miradi ambayo ni safi na salama na kuacha dhana ya kuendelea kutumia maji ya kwenye visima ambayo siyo salama.

Meneja RUWASA Mkoa wa Shinyanga, mhandisi Juliety Payovela, alisema ujenzi wa miradi hiyo ya maji ni wa miezi sita na ujenzi wake unatarajiwa kukamilika juni.

Alitaja vikwazo vinavyowakabili kwenye utekelezaji wa miradi ya maji kuwa ni upatikanaji wa maji ya uhakika hasa katika Halmashauri ya Ushetu na Kishapu pamoja na kuchelewa fedha za malipo za makandarasi na kusababisha kukwamisha kazi kukamilika kwa wakati.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani aliwataka makandarasi hao k wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo, wajiridhishe na ubora wa mabomba, ili kudhibiti upotevu wa maji kunakosababishwa na mabomba kupasuka mara kwa mara.

Mmoja wa makandarasi hao, Mnandi Mnandi kutoka kampuni ya URSINO LTD, alishukuru serikali kwa kuendelea kuwaamini na kuwapatia kazi, huku akiahidi miradi hiyo wataijenga na kuikamilisha ndani ya muda wa mkataba.

# DC ahadharisha safari zisizo za lazima kisa Marburg

**Na Daniel Limbe,** CHATO

SIKU chache baada ya serikali kuthibitisha kuwepo kwa ugonjwa wa Marburg uliosababisha kifo cha mtu mmoja mkoani Kagera, Mkuu wa Wilaya ya Chato mkoani Geita, Louis Bura, amewataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuepuka safari zisizokuwa za lazima.

Kadhalika, amewataka kuendeleza utamaduni wa kunawa na kutumia vitakasa mikono, kuepuka mikusanyiko, kusalimiana kwa kushikana mikono pamoja na kuepuka kushika mizoga ya wanyama, maiti ambazo zimetokea katika mazingira ya kutatanisha.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake huku akisisitiza wananchi kutokuwa na taharuki badala yake waendelee kufanya kazi zao kama kawaida.

Alisema mpaka sasa wilaya hiyo bado haijapokea taarifa yoyote ya mshukiwa wa ugonjwa huo na kwamba hali hiyo haiwezi kuwa sababu ya kubweteka kwa kuwa Wilaya ya Biharamulo na Chato ni majirani na wananchi wake wanatembeleana wakati wote.

"Nitumie fursa hii kuwasihi wananchi waendelee na kazi zao kama kawaida isipokuwa wachukue tahadhari tunazozitoa ili wilaya yetu iendelee kuwa salama" alisema Bura.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chato, Dk. Aristides Raphael, alisema elimu ya afya inaendelea kutolewa kwa jamii hasa kwenye kata zinazopakana na Wilaya ya Biharamulo na Muleba mkoani Kagera ili kuweka udhibiti wa haraka iwapo kutatokea mhisiwa wa ugonjwa huo.

Alizitaja kata hizo kuwa ni Bwongera, Nyarutembo, Kasenga na Katende huku akieleza kuwa baadhi ya zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali ya wilaya hiyo vimewekewa kitengo maalumu cha kupokea wahisiwa wa Marburg iwapo watapatikana.

Kadhalika, aliwataka wananchi kutoa taarifa haraka iwapo mtu atabainika kuwa na dalili zinazoshabihiana na ugonjwa huo ili wataalamu wa afya wachukue hatua za haraka kabla ya madhara makubwa kutokea.

NIPASHE JANUARI 27, 2025

Nipashe

Spotika

KLABU 30 TAJIRI ZAIDI DUNIANI UK. 12-13




# USAJILI BORA WA JANUARI WA WAKATI WOTE LIVERPOOL

**LONDON,** England

DIRISHA la usajili la Januari limethibitisha kuwa soko gumu kulisimamia na wakati mwingine Liverpool wamefanya makosa katika harakati zao za kuongeza nguvu.

Tangu dirisha la majira ya baridi lilipofunguliwa wakati wa msimu wa 2002/03, Liverpool imefanya mikataba mibaya. Andy Carroll, Steven Caulker na Ozan Kabak ulikuwa usajili ambao haukukidhi matakwa yao.

Hawa ndio wachezaji watano bora waliosajiliwa na Liverpool Januari...

**5. Luis Diaz**

Luis Diaz alitekeleza kikamilifu kazi iliyotarajiwa ya kutia saini majira ya baridi. Kufika katikati ya msimu wa 2021/22, Mcolombia huyo alikuwa msaada mkubwa kwa klabu hiyo ya Merseysiders, na kuisaidia kupata Kombe la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alitoa mabao sita na asisti tano katika kipindi chake cha kwanza cha nusu msimu huko Anfield na ameendelea kutoa idadi kubwa zaidi katika miaka yake iliyofuata.

**4. Daniel Sturridge**

Wakati maisha ya Daniel Sturridge yalijaa majeraha ya uchungu na yasiyoisha, fowadi huyo wa kati alikuwa wa kipekee katika umaridadi wake. Liverpool walifurahia kilele cha uwezo wake baada ya kufikia mkataba wa pauni milioni 12 kutoka kwa wapinzani wao Chelsea mwaka 2013.

Sturridge alijivunia mguu wake wa kushoto wenye uwezo wa kuangusha safu ya ulinzi, huku msimu wake wa kwanza kamili Anfield ukimalizika kwa mabao 24 na kutoa pasi saba za mabao katika michuano yote na Liverpool ikikaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England chini ya Brendan Rodgers.

Fowadi huyo wa England akakumbwa na utimamu wa mwili na kuanza kumwathiri, lakini bado alimaliza maisha yake ya uchezaji Liverpool akiwa na mabao 67 katika mechi 160.

**3. Philippe Coutinho**

Ujio wa Philippe Coutinho haukukutana na shangwe kubwa. Kijana huyo wa Kibrazil aliondoka Inter Milan kwa pauni milioni 8.5 tu. Lakini kwa haraka alikuwa mmoja wa wachezaji wa kipekee kwenye Ligi Kuu England.

Coutinho haraka alipata miguu yake huko Anfield, akijipatia sifa kwa nyakati bora. Ustadi na pasi za kugawanya ulinzi zilivutia.

Coutinho alitoa si chini ya mabao 12 na pasi za mabao kwa pamoja katika misimu yake yote minne kamili pale Anfield, na hata akaonekana kuondoka kwa mabadiliko huku Liverpool wakimuuza kwa milioni 142.

**2. Luis Suarez**

Ni vigumu kufikiria kwamba matarajio yalikuwa makubwa zaidi kwa Andy Carroll aliyenunuliwa kwa pauni milioni 35 kuliko Suarez aliyenunuliwa kwa pauni milioni 22.8 wakati wawili hao waliposajiliwa na Liverpool Januari 2011, huku raia huyo wa Uruguay si tu alimpita Carroll kwa kiwango cha ajabu, lakini pia alifanikiwa kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Liverpool.

Ingawa ukorofi wake uwanjani uliharibu sifa yake pale Merseyside kwa kiasi fulani, hakuwezi kuwa na shaka juu ya kipaji cha Suarez. Alifanya jambo lisilowezekana lionekane rahisi kwa ukawaida wa kipekee.

Aliunda ushirikiano wa kutisha na Sturridge aliyetajwa hapo awali wakati Liverpool ilipokaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu wa 2013/14 na alichokosa kwa muda mrefu akiwa Merseyside alikamilisha zaidi kwa matokeo mazuri na uthabiti.

Mabao 82 na asisti 29 katika mechi 133 pekee ndivyo inavyotakiwa kusemwa.

**1. Virgil van Dijk**

Kunaweza kuwa na hoja kwamba hakuna mchezaji aliyesajiliwa ambaye amekuwa na mabadiliko makubwa katika historia ya Liverpool kuliko Virgil van Dijk. Kulikuwa na alama za maswali juu ya ada yake ya uhamisho iliyovunja rekodi ya pauni milioni 75.

Beki huyo mahiri alifanya kupambana na washambuliaji wa kati mahiri zaidi duniani kuonekana si kitu kikubwa, na ameanzisha ushirikiano wa kuvutia na wale wote ambao wamekuwa wakijipanga pamoja naye mara kwa mara katikati mwa safu ya ulinzi.

## ISIKUPITE




HAT-TRICK aliyofunga Kylian Mbappe wakati Real Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye LaLiga juzi dhidi ya Real Valladolid, inamfanya kufikisha mabao 15, moja nyuma ya kinara wa ufungaji hadi sasa, Robert Lewandowski wa Barcelona, lakini pia akifikisha mabao 22 kwenye mashindano yote msimu huu.

## Extra Time

# KLABU 30 TAJIRI ZAIDI DUNIANI




Baadhi ya wachezaji wa Real Madrid wakishangilia ushindi wa mabao 3-0 kwenye LaLiga juzi dhidi ya Real Valladolid. Klabu hiyo imetajwa kuongoza kwa utajiri duniani kwa mujibu wa Kampuni ya Utafiti wa Michezo ya Deloitte Football Money. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON,** England

WACHEZAJI wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani wamebainika huku Ligi Kuu England (EPL), ikiendelea kutawala.

Kampuni ya Utafiti wa Michezo ya Deloitte Football Money imechapisha data kuhusu klabu 30 tajiri zaidi duniani ambazo zinajivunia mapato makubwa zaidi katika msimu wa 2023/24, na rekodi mpya iliyowekwa ya euro bilioni moja.

**Hapa tunaziangalia klabu 30 tajiri zaidi duniani kwa mujibu wa Deloitte, twende sasa...**

### NAFASI YA 30-21

Klabu za Ligi Kuu England zinaunda timu nyingi kati ya kumi zinazoongoza, lakini pia hushiriki kwa urahisi ndani ya 30 bora.

Wolverhampton Wanderers, Fulham, Everton na Crystal Palace zimejumuishwa kutoka 29 hadi 26 kwa mpangilio huo, kwa mara nyingine tena kuangazia misuli ya kifedha ya Waingereza.

Brighton & Hove Albion imeendelea kupaa juu (sasa ni ya 21) kutokana na mtindo wao wa kuvutia wa biashara ambao unalenga kununua wachezaji wa bei ya chini na kuuza kwa bei juu. Ushiriki wa 'Seagulls' hao kwenye Ligi ya Europa 2023/24 pia umeongeza mapato.

Flamengo ndio timu pekee nje ya Ulaya iliyojumuishwa katika 30 bora, iliingia kwenye orodha ikiwa na mapato ya chini ya euro milioni 200. Miamba hao wa Brazil watatarajia kucheza Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia msimu huu wa kiangazi jambo ambalo litawapa fedha zaidi.

Benfica ndio timu pekee ya Ulaya nje ya Ligi Kuu tano kushiriki na ipo katika nafasi ya 25. Mapato yao yaliboreshwa mbele ya AS Roma na Napoli za Italia, pamoja na Eintracht Frankfurt ya Ujerumani.

30. Flamengo euro milioni 198.2
29. Wolves euro milioni 206.9
28. Fulham euro milioni 212.2
27. Everton euro milioni 217.6
26. Crystal Palace euro milioni 218.9
25. Benfica euro milioni 224.0
24. Eintracht Frankfurt euro milioni 245.2
23. Roma euro milioni 249.0
22.Napoli euro milioni 253.6
21. Brighton euro milioni 256.8

### NAFASI 20-11

Klabu nyingine tatu za Ligi Kuu England ziko nje ya kumi bora, huku Aston Villa na West Ham United zikishika nafasi ya 18 na 17. Zote zilipata zaidi ya euro milioni 300 msimu wa 2023/24.

Newcastle United ilipata manufaa kwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023/24, na kupata euro milioni 371.8 katika kipindi chote cha kampeni. Hilo ni ongezeko la kuvutia la asilimia 29 kutoka msimu uliopita na watakuwa na nia ya kuongeza mapato zaidi ya kifedha kwenye Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Soka la Ufaransa haliko katika hali nzuri zaidi ya kiafya, lakini mabeberu wa jadi, Lyon na Marseille zote zimo katika 20 bora. Timu hizo zilifurahia msimu wa 2023/24 wenye matokeo mazuri, huku mapato yao yakiongezeka kwa asilimia 33 kutoka msimu wa 2022/23.

Inashangaza kwamba hakuna timu za Italia zilizojumuishwa katika kumi bora, huku AC Milan, Inter na Juventus zikiwa chini ya jedwali. Miamba wa Turin ni miongoni mwa timu chache ambazo zilipoteza fedha msimu uliopita - euro milioni 78.2 kuwa sahihi - na zimeporomoka hadi nafasi ya 16, huku klabu zote mbili za Milan zikifurahia ongezeko la wastani la asilimia tatu ya mapato.

Atletico Madrid iliyopo nafasi ya 12 pia ilifurahia ongezeko la mapato kwa msimu wa 2023/24, lakini mapato yao bado ni madogo ikilinganishwa na wapinzani wao wa LaLiga. Mbio za fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya zilikuwa bora kwa ongezeko la fedha kwa Borussia Dortmund, ambao walipata mapato ya zaidi ya euro nusu bilioni.

20. Lyon euro milioni 264.1
19. Marseille euro milioni 287.0
18. Aston Villa euro milioni 310.2
17. West Ham United euro milioni 322.2
16. Juventus euro milioni 355.7
15. Newcastle United euro milioni 371.8
14. Inter euro milioni 391.0
13. AC Milan euro milioni 397.6
12. Atletico Madrid euro milioni 409.5
11. Borussia Dortmund euro milioni 513.7

### NAFASI YA 10-1

Klabu sita za Ligi Kuu England 'wakubwa sita' zote zimeingia kwenye kumi bora na timu ya Chelsea iliyokuwa na matumizi makubwa zaidi imepata fedha kidogo zaidi. Ilipata euro milioni 545.5 katika mapato msimu uliopita, chini ya wapinzani wao wa London Tottenham Hitspur ambao walitengeneza euro milioni 615.

Liverpool imeporomoka hadi nafasi ya nane katika viwango vya ubora, ikiachwa na Arsenal ambayo imeruka kutoka nafasi ya kumi hadi ya saba. Majukumu hayo yanaweza kubatilishwa hadi mwisho wa kampeni ya sasa, lakini ongezeko la mapato la asilimia 35 kwa 'Washikabunduki' hao litafurahisha uongozi wa klabu hiyo.

Barcelona na Bayern Munich ziko karibu sana katika nafasi ya sita na ya tano, na hali mbaya ya kiuchumi kwa 'Wakatalunya' hao imewafanya kupoteza euro milioni 39.8 kuliko ilivyokuwa 2022/23. Bayern huwa wanapata mapato thabiti na wamepanda katika viwango licha ya masuala yao ya uwanjani msimu uliopita.

Manchester United inaweza kuwa katika hali mbaya uwanjani, lakini imepanda kwenye orodha kutokana na ongezeko lao la mapato la euro milioni 24.9. Hata hivyo, bado inacheza na wapinzani wao, Manchester City, ambao walipata euro milioni 67.2 zaidi ya 'Mashetani Wekundu' msimu uliopita wakiwa njiani kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England.

Paris Saint-Germain kwa sasa ipo katika nafasi ya tatu kutokana na kuondoshwa kwa nyota wao wakuu katika miaka ya hivi karibuni, lakini hakuna anayekaribia kuinasa Real Madrid.


Mabingwa hao watetezi wa Ulaya waliimarishwa na ukarabati wa Santiago Bernabeu ambao uliwaruhusu kupata mapato ya euro bilioni moja kwa msimu mmoja ambayo ni rekodi mpya.

10. Chelsea euro milioni 545.5
9. Tottenham euro milioni 615.0
8. Liverpool euro milioni 714.7
7. Arsenal euro milioni 716.5
6. Barcelona euro milioni 760.3
5. Bayern Munich euro milioni 765.4
4. Manchester United euro milioni 770.6
3. Paris Saint-Germain euro milioni 805.9
2. Manchester City euro milioni 837.8
1. Real Madrid euro bilioni 1.05

## Nukuu

"Kutolewa kwa kadi nyekundu ni moja ya maamuzi mabaya ambayo nimeona kwa muda mrefu. Kama mwamuzi unaweza kukosea uwanjani, unaweza kuona kitu ambacho si sahihi. Vipi Mwamuzi wa VAR, Darren England, anadhani kuwa refa ana haki hiyo na hakuna haja ya kumpeleka kwenye skrini," **Mfungaji bora wa Arsenal na mchambuzi wa soka, Alan Shearer, akipinga kadi nyekundu alioneshwa Lewis-Skelly na Refa Michael Oliver katika dakika ya 43 juzi dhidi ya Wolves kuwa si sahihi.**

"Myles Lewis-Skelly yuko umbali wa yadi 10 tu nje ya eneo la wapinzani. Ni lazima iwe kwa vitendo vya rafu, lakini hiyo haionekani kama tabia ya rafu. Ni safari ya kimbinu. Sijawahi kuona hilo maisha yangu nimeshangazwa na kadi nyekundu," **Winga wa zamani wa Chelsea na Scotland, Pat Nevin**



"Kwa hakika si kadi nyekundu kwangu. Ninaona sasa kwa mechi nyingi marudio kwa nini ni jambo sahihi kufanya. Labda mwamuzi anaona kwamba Myles Lewis-Skelly hana nia ya kucheza mpira." **Ni wakati mgumu kwa Arsenal kwa kijana, nadhani anahitaji kuelewa kuna njia tofauti za kufanya hivyo," Beki wa kati wa zamani wa Manchester City, Nedum Onuoha**

"Hiyo sio nyekundu, ambayo itapinduliwa haraka sana. Anajaribu kusimamisha shambulio la kaunta na haionekani mbaya sana kwangu," **Mtangazaji wa moja kwa moja wa BBC Radio 5, Mark Chapman: "Kushtua na upuuzi"**

"Bado nina wasiwasi na hilo. Siamini kwamba amemtoa nje," **Kiungo wa kati wa zamani wa Blackburn na Tottenham, Tim Sherwood.**



RAMOVIC

# MAKOCHA WATANO WAPYA KIKAANGONI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea kutimua tena vumbi, Februari Mosi, mwaka huu, kwa baadhi ya timu kuanza mzunguko wa pili na zingine kuendelea pale zilipoishia baada ya kucheza michezo 16.

**Mpaka mzunguko wa kwanza unamalizika, baadhi ya makocha wameshaoneshwa mkono wa kutokea baada ya kufanya vibaya kwenye michezo yao.**

Baadhi yao ni Mwinyi Zahera aliyekuwa Namungo FC, Francis Kimanzi (Tabora United), Paul Nkata, (Kagera Sugar), Mbwana Makata (Prisons) na Mohamed Muya wa Fountain Gate na wengineo.

Mechi chache kabla ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, pia kuelekea wa pili, baadhi ya timu zimepata makocha wapya ambao watakuwa na kazi kubwa ya kufanya kile ambacho wameletwa kukifanya.

Kila kocha ameletwa kwenye timu kutokana na malengo ya klabu husika. Kwa maana hiyo makocha hao wapo kikaangoni wakiangaliwa na uongozi ni namna gani wanavyotekeleza malengo ya klabu kutokana na makubaliano.

Hawa hapa ni makocha sita waliozichukua timu hivi karibuni wakiwa na kazi ya kuzipeleka kwenye nchi ya ahadi...

**1# Sead Ramovic - Yanga**

Aliichukua timu mikononi wa Miguel Gamondi baada ya kupoteza michezo miwili ya Ligi Kuu, ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC na 3-1 dhidi ya Tabora United.

Ameingia kwenye Ligi Kuu kwa kishindo, akishinda mechi nne mfululizo, mabao 2-0 dhidi ya Namungo, 3-2 dhidi ya Mashujaa, 4-0 dhidi ya Prisons, idadi kama hiyo ya mabao dhidi ya Dodoma Jiji, na 5-0 dhidi ya Fountain Gate.

Pamoja na ushindi huo, bado baadhi ya mashabiki wa wamekuwa na wasiwasi na kiwango cha timu hiyo, kinachoonekana kupanda na wakati mwingine kushuka.

Kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, kumezidi kuwaongezea wasiwasi Wanayanga.

Ramovic, raia wa Ujerumani, anachotakiwa kufanya ni kuiongoza Yanga kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la FA kama alivyofanya mtangulizi wake.

Iwapo, timu hiyo itazidiwa kwa idadi kubwa ya pointi kwenye michezo ya mzunguko wa pili na watani zao wa jadi, Simba au Azam, itakuwa hatari kwake, kipigo kwenye 'dabi' kinaweza pia kumuondoa mapema kabla ligi kumalizika.

Anaweza kuendelea kuwapo kama pointi zitakuwa zinaachana kidogo kama ilivyo sasa na hatma yake itaamuliwa na matokeo yatakayopatikana mwishoni mwa ligi.

**2# Hamdi Miloud - Singida Black Stars**

Inawezekana ni kocha aliye kwenye kikaango kinachochemka zaidi kuliko wengine. Ni kutokana na tabia ya klabu aliyopo kutimua makocha mara kwa mara, haijalishi kama amehudumu kwa muda mfupi.

Singida Black Stars, ndiyo timu inayoongoza kwa kutimua makocha wengi mpaka sasa nchini, wakati mwingine kwa sababu ambazo hata hazijulikani vizuri.

Hamdi, mwenye uraia wa Algeria na Ufaransa, ataanza kukiongoza kikosi hicho kwenye mzunguko wa pili, baada ya kuchukua nafasi ya Mbelgiji, Patrick Aussems, ambaye aliondolewa mwishoni mwa mwaka jana kwa kile kilichoelezwa kutofanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu.

Siku zote hizi, timu hiyo ilikuwa ikikaimiwa na Ramadhani Nswanzurwimo hadi alipowasili kocha huyo.

Malengo aliyopewa na klabu ni kupata moja ya nafasi nne za juu ili kucheza mechi za kimataifa msimu ujao. Kama timu itafanya vibaya kwenye mechi chache tu za mzunguko wa pili hawezi kudumu. Kama haitafanya vizuri na mwishoni kushindwa kuipata hata nafasi ya nne, sidhani kama msimu ujao atakuwapo.

**3# Vladislav Heric - KenGold**

Vladislav ndiye kocha mpya wa KenGold, akichukua nafasi ya Omari Kapilima, ambaye amerudishwa kuwa kocha msaidizi. Raia huyu wa Serbia, atakuwa na kibarua kizito cha kuitoa KenGold shimoni na kuibakisha Ligi Kuu.

Klabu hiyo haina malengo makubwa sana, zaidi ya kuibakisha tu Ligi Kuu. hata hivyo inaweza kuwa ni kazi pevu kama watakuwa wamekosea kwenye usajili wa dirisha dogo.

KenGold ndiyo timu iliyosajili wachezaji wengi zaidi kwenye dirisha hili, ikiingiza 22 kwa kuamini kuwa wanaweza kuwa muarobaini wa timu hiyo inayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza nchini, ili kubakia.

Inaburuza mkia, hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikiwa na pointi sita tu kwa michezo 16 iliyocheza, ikishinda mmoja, sare tatu na kupoteza mechi 12.

Kama akiweza hilo, basi kocha huyo atabaki, lakini hali ikiwa vinginevyo anaweza asimalize ligi, au kuagana naye mwishoni.

**4# Josiah Aman i- Prisons**

Josiah, amepewa mikoba ya kuinoa Prisons kuelekea mzunguko wa pili, baada ya kuondolewa kwa Makata kutokana na timu kuonekana kufanya vibaya.

Kocha huyo Mtanzania, awali alikuwa akiifundisha Geita Gold iliyo Ligi ya Championship, atakuwa na kazi moja tu ya kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu. Kinyume cha hapo, safari inamkumba, kabla au mwishoni mwa msimu kama misheni hiyo haitokamilika.

Prisons ipo nafasi ya 13 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 14, kwa michezo 16 iliyocheza mpaka sasa.

**5# Robert Matano - Fountain Gate**

Ataanza kuonekana rasmi mzunguko wa pili akiifundisha Fountain Gate kwa kusaidiana na Amri Said.

Matano, raia wa Kenya, amechukua nafasi ya Muya, ambaye alitimuliwa muda mfupi tu baada ya timu yake kuchabangwa mabao 5-0 dhidi ya Yanga, Desemba 29, mwaka jana.

Kazi yake haitokuwa kubwa sana, bali ni kuendelea kung'ang'ania kuwa nafasi za katikati ya msimamo wa ligi ili kuibakisha timu Ligi Kuu.

Kati ya makocha wote ambao wamepewa malengo ya kuzibakisha timu Ligi Kuu, Matano hana presha sana kwa sababu kikosi chake kipo nafasi ya sita ya msimamo kikiwa na pointi 20 kwa michezo 16 iliyocheza.

Kama atakiongoza kumaliza kwenye nafasi nne za juu itakuwa ni bonasi kubwa, lakini mkakati wa klabu ni kuibakisha, timu ambayo ni rahisi kama akichanga karata zake vizuri. Kitendo chochote cha kuitoa nafasi hiyo na kuishusha chini kunaweza kumfanya kutimuliwa kabla hata ligi haijamalizika.

## JE, WAJUA?



BAO la mkwaju wa penalti alilofunga Romelu Lukaku dakika ya 69 wakati Napoli ikishinda 2-1, limehitimisha rekodi ya kutopoteza mechi hata moja msimu huu kwenye Serie A kwa Juventus. Juve ilicheza mechi 21 za ligi hiyo bila kupoteza kabla ya juzi Napoli kuhitimisha rekodi hiyo.



# TCRA kugawa kwa mnada masafa ya mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema itagawa kwa mnada masafa ya mawasiliano ya simu na intaneti Julai mwaka huu.

Ni hatua ya kiusimamizi itakayochangia kuharakisha ajenda ya uchumi wa kidijitali nchini, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari amesema.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki, akieleza kuwa mnada huo utahusisha vitalu vinne vya masafa katika bendi ya 3600-3800 MHz.

Alisema matumizi ya masafa hayo yataendeleza miundombinu ya mawasiliano ya simu na intaneti ya kasi ambayo itachochea maendeleo ya uchumi wa Tanzania, ambayo ni kwa ajili ya kuwezesha ukuaji wa sekta zote.

"Manufaa mengine ni uwezeshaji shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye utoaji huduma kama vile elimu, afya, kilimo, biashara, huduma za kifedha kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)," alisema.

Dk. Bakari alitaja manufaa mengine kuwa ni kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji na kupanua utoaji huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa watanzania wengi zaidi.

"Matumizi ya masafa hayo pia yatakuza, kuimarisha na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya za TEHAMA na matumizi yake," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, serikali ina malengo ya kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi (broadband) kutoka asilimia 45 mwaka 2020 hadi asilimia 80 mwaka 2025.

Alisema serikali imepanga kuwa kati ya 2020 na 2025 watumiaji intaneti waongezeke kutoka asilimia 43 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2025.

"Mnada huu wa masafa unatarajiwa kuongeza wigo wa mawasiliano na kuwafikia wananchi wengi. Vilevile, matumizi ya masafa hayo yanatarajiwa kuongeza mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye Pato la Taifa kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA," alisema.

Vilevile, alisema masafa hayo yanawezesha serikali kufikia mipango yake ya kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi, kuanzisha huduma za mawasiliano za intaneti ya kasi (broadband) katika maeneo ya umma, yanayojumuisha hospitalini, taasisi za elimu na vituo vya usafiri hadi kufikia asilimia 40 mwaka 2025 na kuunganisha taasisi zake na miundombinu ya mtandao wa kasi.

Dk. Bakari alisisitiza TCRA itaweka masharti ya usambazaji na utoaji huduma kwa matumizi ya masafa husika.

Alisema TCRA itawashirikisha wadau kwenye mchakato wa mnada huo na imeweka ratiba itakayofuatwa kati ya Februari na Juni mwaka huu.

"Hii inalenga kuwawezesha wadau kujipanga kwa mnada huo. TCRA itaanza kwa kuchapisha Februari mwaka huu Rasimu ya Waraka wa Taarifa ya Ugawaji Masafa kwa njia ya ushindani," alisema.

Mnada huo wa masafa wa Julai mwaka huu utakuwa wa tatu kufanywa na TCRA na wa pili kuendeshwa na wataalam wake bila ushiriki wa mshauri mwelekezi.

Oktoba 2022, TCRA iliuza kwa mnada vitalu 11 vya masafa kwenye bendi ya megahezi (Mhz) 700z Mhz 2300, Mhz 2600 na Mhz 3500.

Mnada huo ambao ulipangwa na kusimamiwa na timu ya ndani ya TCRA, ulikuwa wa viwango vinavyokubalika kimataifa, kuanzia mwanzo hadi hatua ya kuuza na kutoa masafa kwa walioshinda.

"Masafa haya yanavutia zaidi watoa huduma kwa kasi na ufanisi. TCRA ilifanya mnada wa kwanza wa masafa mwaka 2018," alisema.

# Basi lagonga lori, utingo afariki, 10 wajeruhiwa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

KONDAKTA wa basi la kampuni ya Premier amefariki dunia na watu wengine 10 kujeruhiwa baada ya basi hilo kuligonga lori kwa nyuma.

Imeelezwa kuwa lori hilo lilikuwa limeegeshwa pembeni mwa barabara kutokana na kuharibika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amoni Kakwale, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema ajali hiyo ilitokea Januari 25 mwaka huu saa nne asubuhi katika kijiji cha Nkuhi, wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Alisema basi hilo lenye namba za usajili T 853 DHA ambalo lilikuwa linatokea Mbeya kwenda Mwanza, liligonga kwa nyuma lori lililokuwa limeegeshwa likiwa na tela lake ambalo lilikuwa linatokea Dar es Salaam kwenda Kigali, Rwanda.

Kamanda Kakwale alimtaja kondakta wa basi aliyefariki dunia kuwa ni Hamis Juma (27), mkazi wa Singida, majeruhi saba walelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida na wengine watatu katika Hospitali ya Wilaya ya Ikungi.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa basi kutochukua tahadhari na kuligonga lori hilo kwa nyuma. Dereva wa basi alitoroka baada ya ajali kutokea. Dereva wa lori naye ametoroka.

**"Jeshi la Polisi linaendelea kuwasaka madereva wote wawili ambao walitoroka baada ya ajali na tunatoa saa 12 wajisalimishe katika kituo cha polisi na hata wasipojisalimisha watasakwa**

"Jeshi la Polisi linaendelea kuwasaka madereva wote wawili ambao walitoroka baada ya ajali na tunatoa saa 12 wajisalimishe katika kituo cha polisi na hata wasipojisalimisha watasakwa popote walipo," alisema.

Kamanda Kakwale aliwataka madereva wanapoendesha magari, kuzingatia sheria za barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima. Muuguzi kiongozi wa zamu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida,Tabitha Mkumbo, alisema walipokea majeruhi saba wa ajali hiyo na mwili wa kondakta huyo ambaye miguu yote miwili ilikuwa imekatika.

Aliwataja majeruhi hao ambao wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo kuwa ni Reoben Msigwa (32), mkazi wa Mwanza, Monga Kaluta (36) ambaye ni dereva wa basi mkazi wa Igoma Mwanza ambaye alikuwa amelala wakati basi linaendeshwa na dereva mwenzake aliyemtaja kwa jina la Musa. Majeruhi wengine ni Hassan Shugape (31), mkazi wa Musoma; Aneth Samweli (18), mkazi wa Puma mkoani Singida; Razaki Ramadhani (28), mkazi wa Iyunga jijini Mbeya; Janeth Sambalu (35), mkazi wa Mafinga mkoani Iringa; na Aisha Omary (22).




Baadhi ya abiria wanaotumia treni ya mwendokasi (SGR), ya Shirika la Reli Tanzania (TRC), wakiteremka katika kituo cha Dodoma mwishoni mwa wiki. Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, zaidi ya abiria 1,500,000 wameshatumia usafiri huo, tangu ulipoanzishwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# MSD yakabidhi vifaatiba Hospitali Wilaya ya Itigi

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

BOHARI ya Dawa (MSD) imetoa vifaa tiba vya Sh. milioni 210 katika Hospitali ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida, ambayo inatarajiwa kuzinduliwa na kuanza kutoa huduma za matibabu Februari 2025.

Meneja wa MSD Kanda ya Kati, Mwanashehe Jumaa, alikabidhi vifaa hivyo juzi kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Vicent Mashinji.

Jumaa alitaja baadhi ya vifaa vilivyotolewa ni mashine ya usingizi, vitanda kwa ajili ya kujifungulia wajawazito, taa za kufanyia operesheni, mashine ya kufanyia usafi na friji ya damu.

Vingine ni mashine za kupima uzito kwa watoto wanaozaliwa ambayo ina uwezo wa kumpima mtoto uzito na urefu, mashine ya kusaidia wagonjwa kupata hewa tiba, meza na mashine ya kufulia nguo.

Meneja huyo alisema vifaa hivyo vilivyotolewa ni baadhi tu kati ya vifaa vya Sh.milioni 300 ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ilitoa maombi na kwamba vilivyobaki vitaletwa ili lengo tarajiwa la kuimarisha huduma za afya linafikiwa na kuhakikisha uzazi unakuwa salama.

"Tunamshukru Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha za kununulia vifaa hivi ambavyo vitasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk.Mashinji, alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha maendeleo yanakwenda kwa wananchi ambapo sekta ya afya katika wilaya hiyo hakuna mwananchi anayetembea umbali wa kilometa tatu kufuata huduma za matibabu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Ayoub Kambi, alisema vifaa hivyo vilivyotolewa na MSD vitasaidia kuondoa changamoto kwa wananchi katika kupata huduma za matibabu hospitali hiyo itakapoanza kutoa huduma rasmi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Hassan Simba, alisema hospitali hiyo ambayo itaanza kutoa huduma Februari mwaka huu hadi sasa zimeshatumika Sh.bilioni 1.750 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba na kwamba watumishi 42 watakaoanza kutoa huduma tayari wameshaletwa.





# Mamalishe wachanga mil. 2.3/- kumwezesha Rais Samia

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

VIKUNDI vya kijamii mkoani Njombe wakiwamo mamalishe wameendesha harambee ya kukusanya Sh. milioni 2.3 kwa ajili ya kumwezesha Rais Samia Suluhu Hassan achukue fomu ya kuwania urais katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Hatua hiyo ni kufuatia Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama cha Mapinduzi CCM uliofanyika wiki iliyopita jijini Dodoma ambao ulimpitisha Rais Samia kuwa mgombea pekee wa urais kwa tiketi ya chama hicho na Dk. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika mkutano maalumu wa kuunga mkono maamuzi ya mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga alisema yamefanyika mambo makubwa ya utekelezaji wa ilani ya chama wakati wa utawala wa Rais Samia.

"Mwaka 2025 tunataka tushikane mikono, tupendane ili kuhakikisha tunampa ushindi wa kishindo Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Sanga.

**"Mwaka 2025 tunataka tushikane mikono, tupendane ili kuhakikisha tunampa ushindi wa kishindo Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Sanga.**

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Njombe, Julias Peter alisema CCM mkoani humo kinatoa tamko la kuunga mkono juu ya uamuzi wa mkutano huo mkuu taifa uliofanyika jijini Dodoma wa kumteua kuwa mgombea pekee wa urais Dk. Samia Suluhu Hassan mwaka huu.

Chifu wa kabila la Wabena, Charles Mkongwa alisema wanaunga mkono maamuzi ya chama ya kupitisha majina hayo kwasababu wamekuwa na uongozi bora unaosikiliza na kutatua kero za Watanzania zilizowasumbua kwa miaka mingi katika sekta mbalimbali.

Mjumbe wa Baraza Kuu Wazazi Taifa, Rabson Mahenge alisema sababu ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ni kwamba amefanya mambo mengi katika kipindi chake cha miaka minne ikiwemo eneo la afya.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Njombe, Dk. Scholastika Kevela alisema wanawake wa mkoa huo na Tanzania kwa ujumla wanajivunia kushika dola kikatiba.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akikabidhi tuzo ya mlipaushuru na tozo bora kwa Mkurugenzi Mtendaji wa M.M Integrated Steel Mills Ltd, Pawan Subhash PateL, wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Mlipakodi Bora wa mwaka 2023/24 jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC aagiza huduma kuboreshwa Hospitali ya Rufani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BODI ya Hospitali ya Rufani mkoani Njombe imetakiwa kusimamia ubora wa huduma za afya pamoja na kuibua miradi ya maendeleo ili kuifanya kuwa ya mfano.

Rai hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omari alipomwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka katika uzinduzi wa Bodi ya Hospitali ya Rufani itakayodumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

Judica alisema ni muhimu kwa bodi hiyo kushirikiana na uongozi wa hospitali katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ambayo italeta tija.

"Tunatakiwa kuifanya hospitali hii kuwa ya mfano hapa nchini kwa mawazo chanya yatakayosaidia katika ujenzi wa taasisi hii," alisema Judica.

Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, Balozi Danford Mpumilwa aliahidi kuwa chombo hicho kitakuwa kichocheo cha maendeleo makubwa kwa kipindi chao cha utumishi.

Kwa upande wake, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, Gilbert Kwesi alisema ushirikiano kati ya wajumbe na uongozi wa hospitali utakuwa nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya taasisi hiyo.

Kwesi alisema kwa sasa hospitali hiyo inatoa huduma zote muhimu na kuiomba serikali kuongeza wataalamu katika fani za vipimo, ili vifaa vilivyopo viweze kutumika ipasavyo badala ya kutumia wataalamu wa mbali kwa njia ya mtandao kusoma vipimo walivyofanya.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Juma Mfanga, aliitaka bodi kuunga mkono juhudi za kupambana na udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano mkoani humo.

# Wataja sababu zinazoua kilimo cha chai

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KUTOLIPWA fedha kwa wakulima na wafanyakazi katika sekta ya chai mkoani Njombe kumetajwa kuwa ni chanzo kwa baadhi ya wakulima kutelekeza mashamba na kujielekeza katika mazao mengine.

Baadhi ya viwanda hivi mkoani Njombe havifanyi kazi na vingine kushindwa kuwalipa wakulima na wafanyakazi wao hatua iliyochagiza wakulima kukiona kilimo hicho hakina tija.

Hayo yaliibuka mwishoni mwa wiki katika kikao cha ushauri Wilaya ya Njombe DCC ambapo baadhi ya wadau wa chai na wakulima wamevitupia lawama viwanda na wawekezaji wa chai, huku wakitaka hatua kuchukuliwa ili kunusuru adha kwa wakulima na wafanyakazi.

Mmoja wa wadau hao, Lukule Mponji alisema Tanzania inahujumiwa katika sekta ya chai na kuwakandamiza wakulima na hivyo kushauri wawekezaji wababaifu waondolewe haraka.

Yotham Mhiche alisema migomo ya wafanyakazi kwenye viwanda vya chai mkoani Njombe imekuwa ya mara kwa mara ambayo inasababishwa na kucheleweshewa mishahara yao

Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swalle alipendekeza kuundwa kwa tume itakayochunguza mkwamo wa viwanda vya chai Njombe ili kupata suluhu ya kudumu ambayo itanusuru sekta hiyo.

"Nakuomba Mkuu ya Wilaya ya Njombe kutoa maelekezo maalumu kwa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kwani wamekuwa wakikata umeme mara kwa mara na kusababisha chai kutosagwa huko Lupembe jambo linalowaingiza kwenye hasara kubwa wakulima," alisema Swalle.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai nchini, Theofhord Ndunguru alisema kuporomoka kwa soko hilo duniani ni kutokana na kushuka kwa unywaji wa chai kuliko uzalishaji.

Alisema hali hiyo imesababisha adha kubwa kiuchumi jambo linalosababisha wakulima na wafanyakazi wengi kulalamika.

"Viwanda vingi vya chai duniani vikiwemo vya Kenya Uganda na Tanzania vimefungwa kutokana na hasara kubwa ya uendeshaji," alisema Ndunguru.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Kiwanda cha Chai Kampuni ya DL, Jaherson Moturi alikiri kuchelewesha malipo ya wafanyakazi wa kiwanda cha chai Kibena na kwamba wanadaiwa mishahara ya mwezi mmoja ambayo wanatarajia kuilipa hivi karibuni.

Alisema katika kiwana cha Ikanga Lupembe wanadaiwa miezi miwili.

Kutokana na changamoto hizo, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alilazimika kuunda kamati maalumu ya uchunguzi itakayofanya kazi ya kufuatilia changamoto za viwanda vya chai ili ije na majibu sahihi yatakayowasaidia wakulima na wafanyakazi.



# Tahadhari yatolewa usimamizi, utunzaji rasilimali zisizo rejesheka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Nishati na Madini Zanzibar, Sayyiomar Abdallah Idarus, amesema rasilimali zisizo rejesheka zisiposimamiwa vizuri zitaleta athari za kimazingira na kuathiri maisha ya wananchi wa Zanzibar.

Alitoa tahadhari hiyo juzi wakati akifungua kikao cha majadiliano kwa masheha wa Wilaya ya Kati kuhusu matumizi sahihi ya rasilimali zisizo rejesheka.

Alisema rasilimali zisizo rejesheka zina umuhimu mkubwa kwa maisha ya wananchi hivyo kuna kila sababu kulindwa na kuhifadhiwa wakati wote, ili kuendelea kudumu kwa muda mrefu.

Alisema kuwa uchimbaji wa rasilimali upo kwa mujibu wa sheria na kuna maeneo yametengwa lakini bado kuna changamoto kwa baadhi ya watu kutokufuata utaratibu.

Alisema masheha wanawajibu mkubwa wa kufuatilia jambo hilo kwa vile shughuli hizo zinafanyika katika maeneo hayo, hivyo wakati umefika kuwa wafuatiliaji wazuri juu ya jambo hilo.

"Uchimbaji huu holela wa rasilimali hizi ikiwemo mchanga, mawe ikiwa masheha hamtokuwa na utayari wa kufuatilia jambo hilo athari ya kimazingira itakuwa kubwa" alisema.

Aidha, alisema kwa kawaida uchimbali wa mchanga au kifusi unatakiwa kuacha kilomita moja katika makazi ya watu lakini kwa sasa sheria hiyo haifuatwi na wahusika hufanya mambo yao kienyeji.

Alisema kuwa wizara imejipanga kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinalindwa wakati wote bila ya kumwonea aibu mtu yeyote.

Mkuu wa Divisheni ya Madini Zanzibar, Abdulsatar Maulid Salim, alisema kwa mujibu wa sheria na kanuni uchimbaji wa vifusi au mchanga muhusika anatakiwa kuacha umbali wa kilomita moja katika makazi ya watu.

Alisema kuwa masheha wanawajibu wa kuyajua maeneo yaliyowekwa kwa ajili ya uchimbaji wa rasilimali hizo ili kutoa mwongozo wa eneo linalohusika limekizi vigezo vyote vya kisheria.

Baadhi ya maasheha walioshiriki kikao hicho walisema uchimbaji wa rasilimali zisizo rejesheka katika shehia zao ni mkubwa lakini wachimbaji hufanya shughuli zao nyakati za usiku jambo ambalo ni changamoto kwa upande wao.

Walisema baadhi ya matajiri wa biashara hiyo wana nafasi kubwa katika wilaya kiasi ambacho masheha wanadharauliwa katika majukumu yao ya kazi.

Sheha wa Bambi, Amour Pandu, alisema kuwa rasilimali hizo licha kuwekewa utaratibu wake juu ya uchimbaji lakini baadhi ya madereva hawafuati utaratibu hasa jinsi ya kuuhifadhi kwa kuufunika ukiwa katika gari ikitembea barabarani na kusababisha athari kwa wapita njia.



Naibu Spika, Mussa Zungu (kulia), akishiriki kukata keki, wakati wa sherehe ya kuzaliwa kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, iliyokwenda sambamba na usomaji wa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Dar es Salaam, Abbas Mtemvu, Diwani wa Kivukoni, Sharik Choughule, Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Ilala, Alhaj Said Side na wanachama wa chama hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Idadi matukio udhalilishaji Zanzibar yapungua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya matukio ya udhalilishaji visiwani Zanzibar imepungua kutoka 1,954 kwa mwaka 2023 hadi 1,809 mwaka jana, ikiwa ni punguzo la asilimia 7.4.

Mtakwimu wa Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira, Asha Mussa Mahfoudh alisema hayo juzi wakati akitoa toleo la takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia la mwaka 2024.

Alisema miongoni mwa matukio yaliyopungua ni pamoja na ubakaji yaliyokuwa 923 ambapo mwaka 2024 yalikuwa 833.

Asha alisema kwa upande wa matukio ya ulawiti kwa mwaka 2023 yaliripotiwa 246 ambapo kwa mwaka 2024 yalikuwa 157.

Alisema matukio ya kuingiliwa kinyume na maumbile yaliyoripotiwa mwaka 2023 yalikuwa 90 ambapo mwaka 2024 yaliyoripotiwa ni matukio 71.

Alisema wilaya zinazoongoza kuripotiwa matukio mengi ya ukatili na udhalilishaji ni Magharibi B Unguja ambapo yaliripotiwa matukio 431 ikifuatiwa na Wilaya ya Magharibi A (429).

Alisema kuwa Wilaya ya Magharibi B imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya ubakaji ikilinganishwa na wilaya nyingine ambapo jumla ya matukio ya ubakaji 198 sawa na asilimia 23.8 kati ya matukio yote ya ubakaji yaliripotiwa.

Akitaja hatua zilichokuliwa kwa watuhumiwa wa matukio hayo ya udhalilishaji yaliyoripotiwa mwaka 2024 alisema matukio 882 kati ya1,809 yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi.

Alisema matukio 352 kati ya matukio 1,809 yamepelekwa mahakamani, matukio 290 yameshinda mahakamani.

Aliwataja wahusika waliofanya matukio hayo kwa mwaka 2024 alisema wapita njia walikuwa 1,394, majirani 389, wapenzi 18, walimu wa shule watatu, wajomba wawili, baba mdogo mmoja.

Aidha alisema kwa upande wa matukio waliofanyiwa watu wenye ulemavu kwa mwaka 2024 alisema yalikuwa 11.

Mkurugenzi wa Idara ya Jinsia, Siti Abasi alisema licha ya kupungua kwa matukio hayo lakini bado ipo haja kwa wanaharakati na wadau wengine kujitathmini katika kutafuta njia mbadala ya kuvitokomeza vitendo hivyo.

Wakili wa Serikali kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Huda Othaman alisema bado kuna changamoto ya mashahidi kudanganya wakati wanapotoa ushahidi na kupelekea ushahidi kuwa na kasoro.

# Mbunge aiita MSLAC kuja kutatua tatizo la uraia

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Kilumbe Ng`enda 'ameiangukia' Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC), kutatua shida iliyopo mkoani Kigoma ya watu wengi kukosa uraia wa Tanzania kutokana na utata wa uraia wa wazazi wao.

Alisema tatizo la utata wa uraia mkoani Kigoma ni kubwa kuliko ilivyo katika mikoa mingine, huku akisema shida kubwa inayochangia tatizo hilo ni ukosefu wa elimu ya namna ya kufuata taratibu kwa baadhi ya wananchi ambao kati ya wazazi wao wawili mmoja huwa na uraia wa nchi nyingine.

"Wananchi wetu wengi wanapoteza haki kwa kushindwa kufuata michakato na taratibu za kisheria za kupata haki zao na moja kati ya maeneo wanayosumbuliwa sana ni haki za kiraia, nasema hivyo kwa sababu wapo watu wanakosa baadhi ya haki za kiraia kwa sababu tu wameshindwa kujua utaratibu wa mzazi mmoja ambaye siyo raia wa Tanzania,"alisema Ng`enda.

Aliongeza: "Labda mtu kazaliwa mama ni wa Burundi, baba wa Tanzania, au baba ni wa Burundi, mama ni wa Tanzania au mama ni wa Congo, mama ni wa Tanzania, kwa hiyo kushindwa kujua namna ya kufuata sheria na taratibu ili athibitishwe kuwa ni raia inasababisha aonekane siyo raia na anashindwa kupata kitambulisho cha NIDA".

Pia, alimshukuru Rais Samia kwa kupeleka huduma hiyo ya msaada wa kisheria mkoani Kigoma na akisema anaamini itakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa mkoa huo.

"Tunamshukuru Rais Samia kupeleka huduma hii nchi nzima ili watu wapate haki zao za kisheria. Kwa Mkoa wa Kigoma haki ambazo wananchi wanahitaji ziko nyingi, lakini nimeisema hiyo haki ya uraia kwa sababu inagusa watu wetu wengi sana," alisema.

Mbunge huyo alitoa mfano wa kijana ambaye kutokana na utata huo wa uraia, amekosa kazi Jeshi la Polisi.

Alisema wananchi hao wanapaswa kuelimishwa katika jambo hilo namna ya kufuata michakato na taratibu za kupata haki yao hiyo ya uraia, hususani kukana uraia wa mzazi mmoja ambaye siyo raia wa Tanzania.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk.Damas Ndumbaro, alisema kampeni hiyo inaendelea kufanyika na itashuka katika ngazi za kila halmashauri ili kila mwananchi mwenye tatizo linalohitaji kutatuliwa kisheria lifanyike na kila mtu apate haki yake pale anapostahili kupata haki hiyo.

# Maelfu kunufaika, kampeni msaada kisheria yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** MPANDA

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, imezinduliwa mkoani Katavi, maelfu ya wananchi wakitarajiwa kunufaika na msaada wa kisheria bila malipo kwa muda wa siku 10.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa huo, Mwanamvua Mrindoko, aliwataka wananchi kujitokeza ili matatizo yao yanayohitaji msaada wa sheria yatatuliwe.

Uzinduzi wa kampeni hiyo ulifanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Kashaulili, mjini Mpanda ambako Mkuu wa Mkoa aliwataka watendaji watakaohudumia wananchi katika kipindi hicho, kutowatoza fedha kwa kuwa zoezi hilo litaendeshwa bila malipo.

Mrindoko aliwataka wazazi na walezi wa watoto waliofanyiwa ukatili, kushirikiana na wataalamu wa sheria ili haki itendeke huku akisisitiza kuwa kampeni hiyo inalenga kuimarisha huduma za kisheria hasa kwa waathiriwa wa ukatili wa kijinsia, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu.

Alisema matarajio yake ni kuona migogoro mbalimbali ya kisheria kama vile ya ardhi, ndoa, mirathi, migogoro inayohusiana na ukatili wa kijinsia, migogoro ya kukosa matunzo kwenye familia itakwenda kupungua mkoani humo kwa kiasi kikubwa.

Awali akitoa maelezo ya kampeni hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Franklin Rwezimula alisema lengo kuu la kampeni hiyo ni kulinda na kukuza upatikanaji haki kwa watu wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini.

Dk. Rwezimula alisema kampeni hiyo itahusisha pia utoaji elimu kuhusu haki zinazohusu ardhi, ndoa, mirathi, madai, jinai na haki za binadamu kwa ujumla.

Dk. Rwezimula aliomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi kutoa ushirikiano wa kutosha kwa watoa huduma za msaada wa kisheria ili wawafikie wananchi kwa wakati.

Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Boniface Butondo aliwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi kwa kuwa msaada huo wa kisheria utawasaidia, hasa katika kutatua migogoro iliyosababishwa na sheria kandamizi katika masuala ya mirathi, mashamba na migogoro ya ardhi.

Butondo alisema kuwa pamoja na mafanikio yanayopatikana chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, wananchi wanapaswa kufahamu haki zao za msingi ili waweze kujilinda na kuchangia katika maendeleo ya nchi.

Alisema elimu ya kisheria ni nyenzo muhimu ya kuwawezesha wananchi kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika maisha yao ya kila siku.

# Kauli ya RC Chalamila yawaibua TLS, LHRC

**Na Mwandishi Wetu**

KAULI ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kuwataka wanawake wanaotaka kwenda kujifungua kujigharamia baadhi ya vifaa, imemwibua Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi akidai inawafedhehesha wanawake.

Hivi karibuni Chalamila, akizungumza na wananchi wa Temeke, alisema alipigiwa simu na mwanamke mmoja akilalamika kutakiwa kujinunulia glavu na vifaa vingine vitakavyowasaidia kujifungua na kutakiwa kulipia Sh. 50,000.

"Nikamwambia toka nje chukua bajaji nenda zako nyumbani kamwambie mumeo achukue kisu na mkasi akusaidie kujifungua.

"Akaniambia 'sasa Mkuu wa Mkoa unanijibuje hivyo!' Nikamwuliza 'hospitali wamekwambia nini?'. Haiwezekani hospitali ikawa na vifaa vyote kila siku, kama umetunza glavu kwa wagonjwa bila malipo, ujue zitaisha.

"Unataka mwanao atoke tumboni awe mwanadamu kama wanadamu wengine, basi kubali kununua vifaa ambavyo umeambiwa vimekwisha, changeni ndugu 20,000/- ajifungue. Akichelewa kujifungua kitakachokufa si hospitali bali ni mtoto au wewe (mama) kwa uzembe mdogo ulionao. Temeke hoyee!" Chalamila alisema

Katika ukurasa wake wa X, Rais wa TLS, Mwabukusi aliandika: "Bwana Chalamika... kati ya watu ambao ni 'liability' na dhihaka kwa waliomteua ni wewe. Na kauli kama hizi ziwe funzo kwa wanawake na kuwafanya wawe 'serious' katika upigaji wao wa kura. Ni aibu kuwaadhibu wanawake na kugeuza mimba kuwa 'liability' kwa taifa. Kuzaa na kulijaza taifa ni kazi inayofanywa na mwanamke, tusiwape mzigo wa pili."

Katika ukurasa wa X wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), wameandika: "Tumesikitishwa na kufadhaishwa na kauli za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamika, wakati akihutubia mkutano wa wananchi wilayani Temeke hivi karibuni.

"Si mara ya kwanza kwa ndugu Chalamila kutoa kauli za kutweza na kufedhehesha utu wa mwanamke. Tunatoa wito kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya ndugu Chalamila."

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 27/1/2025

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **27-1-2025** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dodoma kuelekea Singida, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.0**
**Upana - mita 3.0**
**Kimo - mita 5.0**

3. Njia itakayotumika: **Dodoma** hadi **Singida** kupitia Singida **ROAD.**
Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA PIKIPIKI

**ASHA RAMADHANI MAHUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 812 AAP** aina ya **TOYOTA COROLA.** Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 727 BVN** aina ya **SANLG.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/14402/2025.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 31289/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late FRANK RICHARD MGAYA of Line Polisi Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JOHN ELIYA MGAYA NA JANETH KENETH KISEBO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

.....................................................

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of 1, 2025

....................................
**1ST PETITIONER**

................................
**2ND PETITIONER**

**Presented for filling this 12 day of 12,2024**

.................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSARIFIA



**MARIAMU GEORGE KIBILA** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE013420** iliyotolewa Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe **02/03/2018.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/15896/2025.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH OF TANZANIA UNION** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 618 CWC** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER PRADO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/1609/2025.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1347 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANDREA MATHIAS NJUTU**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**REAH ISAYA MAKANDI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of February, 2025.

Dated at KOROGWE this 20 day of January, 2025.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**OTTY JOHNAS MSUKU** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 559 DMM, T 424 ASX na T 744 DWU.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za Polisi: **PHQ/DAR/UBU/70837/2024, PHQ/DAR/UBU/70839/2024, PHQ/DAR/UBU/70833/2024.**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**OTTY JOHNAS MSUKU** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 667 ANT na T 778 DRZ.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za Polisi: **PHQ/DAR/UBU/70831/2024, PHQ/DAR/KIN/9959/2025.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUSSA A. MBAROUK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1377-0557** kilichotolewa **NATIONAL CORRESPONDENCE INSTITUTE** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/PWA/MKU/2479/2025.**

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yapewa saa 48 kusitisha shughuli DRC

**KINSHASA,** DRC

OFISI ya Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imetoa saa 48 kwa serikali ya Rwanda kuhakikisha inasitisha mara moja shughuli zake zote za kidiplomasia nchini humo.

Hayo ni kwa mujibu wa barua maalumu iliyotolewa na ofisi hiyo ya rais, ikieleza kuwa hilo linafuatiwa pia na hatua ya mara moja ya kuwarudisha wanadiplomasia wote wa DRC walioko nchini Rwanda.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inajiri wakati kundi la waasi la M23 linaloungwa mkono na Rwanda likisonga mbele kuelekea mji wa kimkakati wa Goma, ambao ni kitovu cha kiuchumi na kibinadamu kwa eneo hilo, na kwamba unakabiliwa na hatari kutokana na mapigano yanayoendelea.

Pia ilielezwa kuwa hatua hiyo inaonekana kama onyo la mwisho dhidi ya kile ambacho Congo inakiona kuwa ni uingiliaji wa Rwanda katika masuala yake ya ndani kupitia msaada kwa waasi wa M23.

Kadhalika ilielezwa kuwa waasi wa M23 wamekuwa wakisonga mbele kwa kasi, wakiteka maeneo muhimu kama mji wa Sake uliopo kilomita 27 magharibi mwa Goma, huku jumuiya ya kimataifa ikiendelea kutoa miito ya kusitishwa kwa mapigano.

Wakati huo huo, wanadiplomasia walisema mkutano wa dharura wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu kinachoendelea DRC, ambao awali ulikuwa umepangwa kufanyika leo, umeahirishwa hadi Jumapili kutokana na kuongezeka kwa mapigano.

Ilielezwa kuwa mkutano huo ulioombwa na Kinshasa kupitia ombi lililowasilishwa na Ufaransa, utafanyika Februari 2, mwaka huu asubuhi, na kwamba Mkuu wa ujumbe wa Umoja wa Mataifa (UN) wa kulinda amani DRC, Bintou Keita, anatarajiwa kuhutubia.

Ilielezwa kuwa hali ya usalama inazidi kuzorota mashariki mwa Congo, ambako wanajeshi wa kigeni 13 wanaohudumu katika vikosi vya kulinda amani wameuawa katika mapigano ya hivi karibuni.

Waasi wa M23 wameongeza mashambulizi yao kwa lengo la kuuteka mji wa kimkakati wa Goma, mji wenye wakazi zaidi ya milioni moja na utajiri mkubwa wa madini.

Msemaji wa Jeshi la DRC, Jenerali Sylvain Ekenge, alisema kwamba Rwanda imekusudia kuuteka mji wa Goma, akionesha hatari kubwa inayokabili eneo hilo.

Pia ilielezwa kuwa jumuiya ya kimataifa inatarajiwa kuchukua hatua madhubuti kupitia mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili kushughulikia mgogoro huo na kuzuia kuzorota zaidi kwa hali ya kibinadamu na kiusalama mashariki mwa DRC.

**WASIWASI WAONGEZEKA**

Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa Afrika (AU), na Umoja wa Mataifa (UN) zimeelezea wasiwasi wao mkubwa kuhusu hali hiyo, wakitaka Rwanda kuacha kuwaunga mkono waasi hao.

Mkuu wa Sera za Kigeni wa Umoja wa Ulaya, Kaja Kallas alisema Rwanda lazima isitishe msaada wake kwa M23 na kujiondoa. Na kwamba EU inalaani vikali uwepo wa kijeshi wa taifa hilo nchini DRC kama ukiukaji wa wazi wa sheria za kimataifa, Mkataba wa UN, na uhuru wa mipaka ya DRC.

"Mji wa Goma uko chini ya shinikizo kubwa. Tishio la M23 kuiteka mji huo halikubaliki na lina madhara makubwa ya kibinadamu na kiusalama katika eneo hilo," alisema.

Katika hatua nyingine, Rwanda imekanusha mara kadhaa madai hayo, ikisema kuwa haina uhusiano wa moja kwa moja na kundi hilo.

Mgogoro wa mashariki mwa Congo umeendelea kuwa chanzo cha mvutano wa kisiasa na kijeshi kwa miaka mingi, ukichochewa na rasilimali za madini zinazopatikana katika eneo hilo.

Uamuzi wa Congo kurejesha wanadiplomasia wake kutoka Kigali na kuwataka wa Rwanda kuondoka Kinshasa unaashiria kuzorota zaidi kwa uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili jirani.

Hali hii inazidi kulifanya suala la mashariki mwa Congo kuwa mojawapo ya migogoro tete zaidi barani Afrika, likihitaji hatua za haraka za kidiplomasia ili kuepusha mgogoro mkubwa zaidi wa kikanda. **DW**

## Wapalestina wazuiwa kurudi Gaza, mmoja auawa

**GAZA,** Palestina

JESHI la Israel limewafyatulia risasi Wapalestina wanaojaribu kurejea majumbani mwao kaskazini mwa Ukanda wa Gaza na kuuwa mtu mmoja, huku Hamas ikiishutumu Israel kwa kuchelewesha utekelezaji wa makubaliano ya kusitisha mapigano.


Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema hawataruhusu kurejea kwa Wapalestina waliokimbia makazi yao kutokana na kuchelewa kwa Hamas kumwachilia mateka mwanamke ambae ni raia wa kawaida.

Ilielezwa kuwa asilimia kubwa ya Wapalestina waliokimbia makazi yao wameonesha msisitizo wa kutaka kurejea kaskazini mwa Gaza hata kama eneo hilo ni magofu kutokana na mashambulizi ya kijeshi ya Israel katika kipindi cha miezi 15 iliyopita.

Mkazi mmoja aliyeweka kambi kando ya barabara aliiambia AlJazeera "Tumekuwa hapa kando ya barabara tangu jana usiku, tunataka kurudi, hata kama tunaishi kwenye magofu ya nyumba yetu. Tuko imara kwa sababu sisi ndio wamiliki halali wa ardhi".

Katika hatua nyingine, Wapalestina walilaani pendekezo la Rais wa Marekani Donald Trump la kuwahamisha kutoka Gaza hadi Misri na Jordan.

Rais Trump alieleza kuwa amezungumza na mfalme wa Jordan kuhusu uwezekano wa kujenga makazi na kuhamisha zaidi ya Wapalestina milioni moja kutoka Gaza hadi katika nchio hiyo ya jirani. **BBC**



Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron (katikati) baada ya kujaribu kuwapatanisha Rais wa Rwanda Paul Kagame (kushoto) na Rais wa DRC Felix Tshisekedi bila mafanikio. **PICHA: MTANDAO**

## SADC yalaani mauaji ya vikosi DRC

**KINSHASA,** DRC

JUMUIYA ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) imelaani mauaji ya vikosi vyake yaliyotekelezwa na M23 mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na kutaja mashambulizi hayo kama kitendo cha uchokozi.

Awali ilielezwa kuwa wanajeshi 13 wanaohudumu na vikosi vya kulinda amani katika DRC wameuawa katika makabiliano na waasi wa kundi la M23.

Taarifa ya jumuiya hiyo iliyotolewa jana, haikutoa takwimu ya idadi ya wapiganaji ambao wako chini ya SADC waliouawa au kujeruhiwa, licha ya nchi wanachama zilizothibitisha kifo cha raia wao katika shambulio la M23 lililotekelezwa siku chache zilizopita.

"Kutafuta upanuzi wa eneo kwa M23 kunafanya hali ya kibinadamu na usalama kuwa mbaya zaidi huko Mashariki mwa DRC," sehemu ya taarifa ya SADC ilisema.

Mataifa yaliyojitokeza ni Afrika Kusini iliyosema wanajeshi wake tisa waliuawa, pamoja na Malawi ambayo ilieleza kuwa raia wake watatu wameuawa.

Uruguay ilisema mwanajeshi anayehudumu na ujumbe wa kulinda amani wa UN pia alipoteza maisha katika shambulio la M23, wakati raia wengine wanne walijeruhiwa.

Umoja wa Ulaya (EU) pia ililaani kwa nguvu uwepo wa kijeshi wa Rwanda huko DRC, na kuiita ukiukaji wazi wa sheria za kimataifa, makubaliano ya UN na uadilifu wa eneo la DRC.

"Rwanda lazima iache kusaidia M23 na kujiondoa," Mkuu wa sera ya kigeni ya EU Kaja Kallas alisema.

SADC pia iliwasihi pande zote katika mzozo huo kufuata sheria na masharti ya makubaliano ya amani yaliyopo na kufanya mazungumzo. **BBC**

HABARI MICHEZO

# NYOTA WAPYA WA MWEMBE MAKUMBI CITY KUIVAA JKU LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI timu ya Mwembe Makumbi City ikishuka uwanjani leo kupepetana na Maafande wa JKU SC katika mchezo wa kiporo wa kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi kuu Zanzibar, itaanza kutumia nyota wake wapya, lakini pia ikicheza kwa tahadhari kubwa kutokana na ukosefu wa wapinzani wao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rajab Mrisho, alisema anakutana na timu ambayo inauzoefu mkubwa katika mashindano ya nje na ndani, hivyo lazima aingie kwa tahadhari na heshima ili kufanikisha mpango wake.

**Alisema mbali na uzoefu wa kimashindanao, lakini pia wana wachezaji wazuri wakuelewa mbinu za mchezo mapema.**

Mrisho alisema ingawa wapinzani wao hawapo vizuri katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, hiyo haiwafanyi kubweteka katika michezo hii ambayo timu zote zimeimarisha vikosi vyao kupitia usajili wa dirisha dogo.

Alisema katika kuelekea mchezo huo timu yake itaendelea na mwenendo ule ule walioanza nao mwanzo wa msimu ili kuona wanachokihitaji wanakipata.

"Tunashuka uwanjani kuhakikisha hatupotezi malengo hasa kupata point tatu katika mchezo huu muhimu, tunaenda kupambana na najua si mchezo rahisi, lakini tutashinda," alisema.

Aidha, alisema katika mchezo huo atakuwa na ingizo jipya la wachezaji ambao wamewasajili katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

Kocha huyo alisema kupitia wachezaji wake hao wapya na wale wa zamani, anaamini watafanya vizuri katika mchezo huo muhimu kabla ya kuanza michezo yao ya mzunguko wa lala salama.

Mwembe Makumbi City inashuka uwanjani ikiwa nafasi ya tatu na alama zake 27, wakati wapinzani wao JKU SC wakiwa nafasi ya tisa na alama zao 21.

**FURUKUTA!...**



Beki wa kushoto wa Yanga, Israel Mwenda, akipasua katikati ya msitu wa wachezaji wa Copco FC kwenye mechi ya kuwania kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Yanga ilifuzu hatua hiyo kwa kushinda mabao 5-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Makambo sasa aipania Simba*

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Tabora United, Heritier Makambo, amesema yeye na wachezaji wenzake wanaendelea kujiandaa kikamilifu kuivaa Simba kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi Februari Mosi, mwaka huu, akitamba kuwa wanahitaji ushindi kwa hali na mali ili kufikia malengo yao.

Akizungumza jana kutoka Tabora, Makambo straika wa zamani wa Yanga, alisema yeye binafsi amejipanga kuonesha ni jinsi gani ni mchezaji mkubwa, ambaye anaweza kufanya matukio kwenye michezo kama hiyo.

"Mechi hiyo ni ya Ligi Kuu kama zingine tu, tumefanya vizuri mzunguko wa kwanza, tumecheza mechi saba bila kupoteza, lakini haitokuwa mechi rahisi, tutauchukulia kama mchezo muhimu kwa sababu tukipata pointi tatu, itatupa nguvu sana kwenye mzunguko wa pili," alisema straika huyo.

Alisema awali hawakuwa na malengo makubwa kwenye kikosi hicho, lakini baada ya kuona wanapata ushindi mfululizo, yakabadilika na sasa wanataka nafasi nne za juu.

"Mwanzoni hatukuwa na malengo makubwa, lakini baada ya kuwa tunapata ushindi mechi baada ya mechi yakabadilika, sasa tunapambania nafasi ya kwanza mpaka ya nne, ndiyo maana mchezo dhidi ya Simba tumeuwekea maanani sana, tunataka tuoneshe kuwa tunahitaji nafasi za juu, na kila mchezaji na mimi mwenyewe tunataka tuoneshe kuwa tuna uwezo wa kucheza michezo mikubwa kama hiyo," alisema raia huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Utakuwa ni mchezo wa kiporo wa raundi ya 16, huku ukiwa ni wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, ambapo katika mchezo wa mzunguko wa kwanza uliopigwa, Agosti 18, mwaka jana, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Simba ilishinda mabao 3-0.

Wakati Simba ikiongoza ligi ikiwa na pointi 40, Tabora United ipo nafasi ya tano ya msimamo, ikiwa na pointi 25.

## Matano akunwa na kikosi chake Fountain Gate

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu mpya wa Fountain Gate, Robert Matano, amesema ameridhishwa na kikosi chake, ingawa amekiri bado ana kazi kubwa ya kukiunganisha ili kicheze kitimu.

Kocha huyo raia wa Kenya, alizungumza hayo juzi baada ya timu hiyo kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Eagle Sports, kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Sekondari Singe, Mbulu mkoani Manyara, Fountain Gate ilishinda mabao 2-0.

Matano alisema ana wiki mbili tu tangu aanze kukinoa kikosi hicho, lakini amekutana na wachezaji wazuri wenye uwezo akiwa na uhakika kila atakapowaingizia vitu vipya kwenye mazoezi watabadilika.

"Maandalizi ni mazuri, kikosi ni kizuri, nimeridhika na wachezaji, lakini kwangu bado, nataka wafanye zaidi ya hapa, nina wiki mbili tu nadhani mbele ya safari tutaongea mengine, kabla sijaja hapa, nimeifuatilia kwa muda Fountain Gate, ni timu nzuri na inataka kuendelea, na hizi ndiyo zangu, kuzitoa timu chini kuzipeleka juu, ni changamoto kubwa kwangu kwa sababu sijawahi kufundisha nje ya nchi ya Kenya, niko tayari kwa kazi, naahidi kuifanya kuwa tishio kwenye Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Matano amezifundisha Klabu za AFC Leopards, US Nakuru, Sofapaka FC na Tusker zote za Kenya, akiwa na vikombe 11 vya Ligi Kuu ya Kenya.

Hata hivyo, atakuwa na kazi kubwa atakapoanza kibarua chake dhidi ya Simba, mechi inayotarajiwa kuchezwa, Februari 6, mwaka huu, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara.

Mchezaji wa timu hiyo, Amos Kadikilo, amesema wapo kwenye maandalizi kabambe kuelekea kwenye mchezo dhidi ya Simba

"Tuko kwenye maandalizi, hakuna tofauti kubwa sana na maandalizi ya mechi zingine za ligi na hizi timu kubwa, ila unapokwenda kucheza na Simba, Yanga au Azam kinachosisitizwa sana ni umakini, kwa sababu wenzetu kosa moja wanaweza kulitumia, tofauti na timu za madaraja yetu, makosa yanaweza kufanyika mengi na wenzao wakashindwa kuyafanya kuwa mabao," alisema mchezaji huyo.



## ZISIKUPITE

### RASHFORD NA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, yuko tayari kupunguziwa mshahara katika jaribio la kutaka kuhamia Barcelona Januari hii. ***(Daily Star Sunday)***

### NKUNKU AULIZIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27, huku winga wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye miaka 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko. ***(ESPN)***

### ATAKIWA NAPOLI

MKURUGENZI wa Michezo wa Napoli, Giovanni Manna, amethibitisha kuwa klabu hiyo inavutiwa na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 23, lakini akaongeza kuwa miamba hiyo ya Italia "haitalipa bei ambayo haiendani na thamani yake". ***(Football Italia, via DAZN)***

### DORGU KUOTA MBAWA UTD

KLABU ya Manchester United imekuwa na ofa nzuri zaidi ya pauni milioni 27 kwa beki wa kushoto wa Denmark, Patrick Dorgu mwenye umri wa miaka 20, iliyokataliwa na Lecce, ambayo inataka pauni milioni 35. ***(Talksport)***

### IASAK MKATABA MREFU

KLABU ya Newcastle United inapanga kumpa mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25, mkataba mpya wa muda mrefu msimu wa majira ya joto. ***(Sunday Telegraph)***

### DURAN SASA AGOMBEWA

REAL Madrid imeungana na Paris St-Germain na Al-Nassr kutaka kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa na Colombia, Jhon Duran, 21. ***(Footmercato)***

### SESKO ANAITAKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Slovenia, Benjamin Sesko, angependelea kuhamia Arsenal kuliko Chelsea au Manchester United, lakini RB Leipzig hawataki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 katika dirisha hili la uhamisho la Januari. ***(Talksport)***

### BUENDA NA LEVERKUSEN

KIUNGO wa kati wa Aston Villa, Emiliano Buendia anafuatiliwa na Bayer Leverkusen. Klabu hiyo ya Ujerumani inaangalia uwezekano wa kumsajili kwa mkopo na chaguo la kumnunua Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sport Germany)***

### FATI AWANIWA FENERBAHCE

KOCHA wa Fenerbahce, Jose Mourinho, anataka kumsajili winga wa Barcelona, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 22, kwa mkopo ili kuongezea timu nguvu ya kutwaa ubingwa. ***(AS)***

### CASADEI APEWA OFA

CHELSEA imekubali ofa ya euro milioni 12 kutoka Lazio kwa kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 22, katika mkataba unaojumuisha kipengele cha kuuzwa cha asilimia 25. ***(Sport Italia, via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




## MBAPPE: NATAKA UBINGWA WA LALIGA SI MFUNGAJI BORA

**MADRID,** Hispania

KYLIAN Mbappe amesema anajali zaidi Real Madrid kushinda taji la ligi kuliko kumaliza kama mfungaji bora wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kauli hiyo ikija baada ya kufunga 'hat trick' yake ya kwanza katika ushindi wao wa 3-0 dhidi ya Real Valladolid Jumamosi.

**Mbappe alianza kufunga dakika ya 30 - baada ya kugongeana na Jude Bellingham - kabla ya kuongeza bao la pili dakika ya 57 na kisha kufunga penalti kwenye muda wa nyongeza.**

Matokeo hayo yameiacha Madrid kileleni mwa msimamo wa LaLiga ikiwa na pointi 49, nne mbele ya Atletico Madrid inayoshika nafasi ya pili, ambayo ilitoka sare ya bao 1-1 na Villarreal mapema Jumamosi.

"Nimefurahishwa na hat-trick, lakini nina furaha zaidi na ushindi," alisema Mbappe akiiambia Real Madrid TV.

"Ilikuwa muhimu sana kushinda leo (juzi). Baada ya matokeo ya Atleti, kulikuwa na shinikizo zaidi."

Mbappe sasa amefunga mabao 15 ya ligi msimu huu - 22 katika mashindano yote.

Wakizungumza mapema wiki hii, wachezaji wenzake, Vinicius Junior na Rodrygo, walisema wanataka kuhakikisha Mbappe anamaliza msimu kama mfungaji bora wa Ligi Kuu Hispania, ili atwae tuzo ya Pichichi.

"Rodrygo na mimi tutafanya kila tuwezalo ili Mbappe awe mfungaji bora katika kila mashindano, kwa sababu ndiyo maana alikuja hapa," alisema Vinicius.

"Hiyo ni nzuri, lakini naweza kusema ninahitaji kuwasaidia pia," alijibu Mbappe Jumamosi baada ya bao lake la tatu.

**Sote tunataka timu ishinde. si tuzo binafsi, kwa sababu nimefanya hivyo mara nyingi katika...**


"Sote tunataka timu ishinde. Haijalishi mimi kuwa mfungaji bora, kwa sababu nimefanya hivyo mara nyingi katika maisha yangu - lakini kushinda taji la ligi ndio jambo muhimu zaidi kwangu."

Naye kwa upande wa Kocha, Carlo Ancelotti alimtaja Mbappe kama "fowadi bora wa kati duniani."

"Nilisema siku ya kwanza hapa kwamba naweza kucheza katika nafasi zote tatu za ushambuliaji," alisema Mbappe alipoulizwa kuhusu kucheza nafasi ya fowadi wa kati.

"Mabadiliko yangu yameisha kwa hakika. Najisikia vizuri, kwa mienendo yangu, na wachezaji wenzangu, unaweza kuiona uwanjani."

# MO SALAH AIPIKU REKODI YA HENRY EPL




**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah alipanda hadi nafasi ya saba kwenye orodha ya wafungaji mabao wa muda wote wa Ligi Kuu England (EPL), kutokana na bao lake la dakika ya 35 wakati Liverpool iliposhinda 4-1 dhidi ya Ipswich Town kwenye Uwanja wa Anfield Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amekuwa katika kiwango bora kwa kikosi cha Kocha, Arne Slot, ambacho kinaongoza msimamo wa Ligi Kuu msimu huu na alifunga bao lake la 176 akimpita Thierry Henry (175) na moja nyuma ya gwiji wa Chelsea, Frank Lampard (177).

Salah ana mabao mawili mbele ya Erling Haaland wa Manchester City na Alexander Isak wa Newcastle United katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu msimu huu.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri pia ametoa pasi 13 za mabao.

Ushindi wa Liverpool dhidi ya Ipswich uliwafanya wadumishe uongozi wao wa pointi sita dhidi ya Arsenal walio nafasi ya pili kileleni mwa Ligi Kuu England.

Bao la fowadi huyo linamaanisha kuwa sasa anakuwa mchezaji wa pili nje ya Ulaya aliyefunga mabao mengi zaidi katika historia ya Ligi hiyo, nyuma ya Sergio Aguero (184).

Alan Shearer ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Ligi Kuu England akiwa amefunga mabao 260.

Tangu Salah ajiunge na Liverpool msimu wa 2017-18, amefikisha mabao 174 na anashika nafasi ya nne kwa mchezaji yeyote katika ligi tano kuu za Ulaya kufunga mabao mengi (alifungia Chelsea mabao mawili kabla ya kujiunga na Liverpool). Robert Lewandowski (245), Harry Kane (253) na Kylian Mbappé (224) ndio wachezaji pekee ambao wamemzidi Salah kwa mabao mengi tangu msimu wa 2017-18.

Salah yuko katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake hapo Merseyside na yuko huru kufanya mazungumzo na klabu nyingine nje ya England.

Wachezaji wenzake wa Liverpool Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold pia mikataba yao inafikiri mwisho.

# Napoli haitaongeza bei kwa Garnacho

**NAPLES,** Italia

MKURUGENZI wa Michezo wa Napoli, Giovanni Manna, amezungumza kuhusu uwezekano wa kumsajili winga wa Manchester United, Alejandro Garnacho, kabla ya ushindi wa timu yake dhidi ya Juventus Jumamosi, akisisitiza kwamba viongozi hao wa Serie A hawatatoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili kumnunua nyota yoyote.

Garnacho amekuwa miongoni mwa majina yanayohusishwa sana na kuhamia timu hiyo inayonolewa na Kocha Antonio Conte baada ya Khvicha Kvaratskhelia kutimkia Paris Saint-Germain, pamoja na fowadi wa Borussia Dortmund, Karim Adeyemi.




ESPN iliripoti wiki iliyopita kwamba United walikataa ofa ya awali ya euro milioni 50 kutoka Napoli kwa ajili ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina.

Alipoulizwa na DAZN kuhusu maendeleo ya dili lolote kabla ya ushindi wa 2-1 kwenye Uwanja wa Diego Maradona, Manna alisema: "Haya ni majina mawili ambayo yanatuvutia, ni wachezaji tunaowapenda, lakini si wao pekee.

"Tunajaribu kutathmini mambo machache na kuangalia fursa, lakini hakika hatutalipa bei ambazo ziko nje ya thamani ya soko."

"Tulifanya mauzo haya ambayo kwa bahati mbaya yalikuwa muhimu kwa kile mchezaji alitaka na mienendo yetu. Tutaheshimu vigezo vyetu, si tu kwa ada ya uhamisho, lakini pia mshahara.

"Tunatathmini hali chache, haitakuwa sawa kuwapa mashabiki wetu matumaini ya uongo, lakini kwa hakika tutafanya kile ambacho ni bora kuboresha kikosi."

Garnacho bado yuko kwenye mkataba hadi mwaka 2028, na vyanzo viliiambia ESPN kwamba hesabu ya United ni zaidi ya euro milioni 70 ili kumuachia mchezaji hiyo.

Garnacho ameichezea United mara 33 msimu huu katika mashindano yote, akifunga mabao nane na kusaidia matano.

# Arteta akerwa na kadi nyekundu ya Skelly

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema "nimekerwa" na kadi nyekundu ya Myles Lewis-Skelly, lakini akasifu kiwango cha timu yake ya Arsenal katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Wolves Jumamosi ambao uliongeza matumaini yao ya mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

Lewis-Skelly mwenye umri wa miaka 18, alitolewa kwa kadi nyekundu katika dakika ya 43 pale kwenye Uwanja wa Molineux baada ya kumchezea vibaya Matt Doherty umbali wa yadi 30 kutoka kwenye lango la wenyeji na mwamuzi Michael Oliver aliiona kuwa faulo. VAR ilikubali uamuzi huo, na kuiacha Arsenal ikipambana na wachezaji 10 huku matokeo yakiwa bado 0-0.

Lakini namba za wachezaji zikawa sawa katika dakika ya 70 wakati kiungo wa Wolves, João Gomes alipooneshwa kadi nyekundu, na dakika nne baadaye Riccardo Calafiori aliyetokea benchi aliifungia Arsenal bao ambalo lilikuwa pekee kwenye mchezo huo.

Ushindi huo unawaacha Arsenal pointi sita nyuma ya vinara wa ligi Liverpool, ambao wana mchezo mkononi.

"Ni wazi na nitawaachia nyinyi," alisema Arteta kuhusu kadi nyekundu ya Lewis-Skelly. "Nina hasira. Lakini nitawaacha, ni wazi kwamba sidhani kama maneno yangu yatasaidia.

"Ni wazi kwamba labda hata hatuhitaji kukata rufaa."




Alipoulizwa kuhusu umuhimu wa ushindi huo kwa timu yake yenye majeruhi wengi, ambayo haikuwa na nahodha Martin Ødegaard, Arteta alijibu: "Ni ajabu walichokifanya.

"Timu haitasimama, tutaendelea, timu hii ina ari na nia ya kupigana na chochote, walionesha hilo tena leo (juzi)."

## HABARI MICHEZO

## Simba yatoa fundisho FA

INATOKA UKURASA 24

kwa kupigiana pasi fupifupi nyuma, kabla ya kupiga mipira mirefu pembeni ambapo mara kadhaa walifanikiwa kuipenya ngome ya Simba, lakini wachezaji wao, Miraji Sallah, Joseph Sekue, Joachim Limbu, hawakuwa makini.

Mchezaji mwingine aliyeingia kipindi cha pili, Balua, alifunga bao la sita, dakika ya 79 kwa shuti kali la umbali ambalo wengi walidhani kipa Kizuguto angedaka, lakini ulimparaza mikononi na kutinga wavuni.

Baada ya bao hilo timu zote hazikuonekana kama kuna kitu zinasaka tena, zaidi ya kucheza kwa kupoteza muda ili mechi imalizike.

## Ramovic apata pakuzungumzia

INATOKA UKURASA 24

ya tatu ya msimamo wa Kundi A.

Kocha Mkuu wa Copco, yenye maskani yake jijini Mwanza, Lucas Mlingwa, alisema mpango wao kwa kiasi kikubwa ulifanikiwa, kilichotokea kupigwa mabao yote hayo ni kupungua kwa umakini wa wachezaji wake.

"Mimi naona imeenda kama tulivyo 'plan', tupunguze eneo la kucheza, hasa nyuma pale katikati ili tujue wanashambulia kutokea wapi, na tulifanikiwa, tuliamua wapite pembeni si ndani, kipindi cha kwanza tulifanikiwa, hakuna bao lolote lililopitia kati, walilolipata lilikuwa la kona," alisema kocha huyo.

Alisema ubora wa wachezaji wa Yanga na uchanga waliokuwa nao, ndiyo ulioamua mechi hiyo, huku akiwasifu vijana wake kwa kufuata maelekezo aliyowapa.

"Kipindi cha pili kilichotugharimu ni umakini ulipungua, kukaa kwenye mpango kwa dakika 90, kwa wachezaji wadogo hawa ilikuwa ngumu sana, wakawa na fatiki kichwani, lakini mpango wetu leo umekwenda sawa na hata ukiangalia mabao karibuni yote yamefungwa kutokea pembeni na si ndani, nimefurahi kwanza tumefanya kile tulichokubaliana na kimefanyika," alisema.

Yalikuwa ni mabao ya Shekhan Ibrahim, Prince Dube, Maxi Nzengeli, Duke Abuya na Mudathir Yahaya, yakitosha kuiangamiza timu hiyo inayocheza, 'First Legue.'

Wakati Yanga inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 39, Copco FC, iliyoshuka msimu uliopita kutoka Championship, inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa First League, Kundi B , ikiwa na pointi tano kwa michezo saba iliyocheza, katika ligi yenye makundi mawili na kila kundi likiwa na timu nane.

# AZAM: SIMBA, YANGA KUNA POINTI ZETU SITA

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, ameziambia Klabu za Simba na Yanga wanahitaji pointi sita kutoka kwao kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa kirafiki kati ya timu yake na JKT Tanzania juzi, katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, Azam ikishinda mabao 3-2, kocha huyo alisema kwa sababu malengo yao msimu huu ni ubingwa, basi hawawezi kuupata kama hawatokusanya pointi kutoka timu ambazo wanawania nazo taji moja.

"Tumedondosha pointi kadhaa mzunguko wa kwanza, lakini haina maana kuwa hatuwezi kusonga mbele, ligi ndiyo kwanza ipo katikati, bado tuna nafasi na ukizingatia washindani wetu hatujacheza nao mechi za mzunguko huu wa pili, najua tulichukua pointi tatu kutoka kwa Yanga, hilo ni jambo zuri, Simba ndiyo ilitufunga na kuchukua zote, sasa hatuwezi kufanya makosa kudondosha tena dhidi yao, hasa kwa Simba.

"Kwa maana hiyo Simba na Yanga wajue kuwa mzunguko wa pili wana pointi sita zetu, kila mmoja ana pointi tatu ambazo anatakiwa kutukabidhi tukikutana naye," alitamba kocha huyo.

**Alisisitiza kuwa, timu yoyote inayowania taji ni lazima iwe na tabia ya kutokubali unyonge kwa zile ambazo inashindana nazo kulisaka, vinginevyo haitoweza kufanikisha jambo hilo siku zote.**

Alisema kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya KMC, utakaochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Februari 6, mwaka huu.

Katika mechi hiyo ya juzi dhidi ya JKT Tanzania, mabao ya Azam, yalifungwa na Yoro Diaby, aliyepachika mawili, na moja la Alassane Diao, huku ya wenyeji wao yakifungwa na Edward Songo na Abdulrahim Bausi.

Azam ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 36, nyuma ya Yanga yenye pointi 39, juu yake wakiwa vinara Simba wenye alama 40.



Beki wa kati wa Simba, Chamou Karaboue, akimiliki mpira dhidi ya washambuliaji wa Kilimanjaro Wonders, kwenye mechi ya raundi ya tatu ya michuano ya Kombe la FA, iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana na timu yake kushinda mabao 6-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mayanga afunguka kupata tuzo Mbeya City*

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kutangazwa kuwa Kocha Bora wa Desemba, kwenye Ligi ya Championship, Salum Mayanga, anayeifundisha Mbeya City, amezungumza kwa mara ya kwanza akisema tuzo hiyo imempa motisha na morali wa kuirudisha timu hiyo Ligi Kuu.

Mayanga, ambaye ni kocha wa zamani wa Mtibwa Sugar, kwa sasa anainoa Mbeya City, majuzi akitangazwa kuwa kocha bora wa Desemba, huku mchezaji wa timu hiyo, Kilaza Mazoea, akitangazwa kuwa mchezaji bora wa mwezi huo.

"Nashukuru sana vijana wangu, viongozi, na wasaidizi wangu wa benchi la ufundi ambao wamenisaidia hadi kupata tuzo. Hii ina maana kubwa kwangu, itanisaidia sana kupambana kadri ya uwezo wangu ili niirudishe Mbeya City Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Mbeya City ilishuka daraja msimu wa 2022/23 ilipoduwazwa na timu iliyokuwa inachipukia, Mashujaa FC, ikichapwa jumla ya mabao 4-1 katika mchezo wa pili wa mchujo, baada ya kufunga mabao 3-1 ugenini, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, kabla ya kukubali tena kipigo cha bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Akizungumzia mzunguko wa pili ligi hiyo, alisema utakuwa mgumu kwani kila timu itakuwa imejipanga kisawasawa, lakini hiyo haizuii malengo yao waliyojiwekea msimu huu.

"Mzunguko wa pili utakuwa mgumu kimbinu na kiufundi, mategemeo yetu ni kucheza kama wa kwanza, ili kuongeza umakini, tutacheza kwa ari na kujituma, tunataka tushinde mechi nyingi zaidi.

Kwa upande wa usajili, umezingatiwa kwa asilimia 95, kilichobaki ni kwangu mimi na wasaidizi wangu kutengeneza muunganiko wa vijana waliokuwapo na wapya," alisema.

Timu hiyo inashika nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi ya Championship, ikiwa na pointi 34 kwa michezo 15 iliyocheza, ikiwa nyuma kwa pointi saba kwa vinara, Mtibwa Sugar ambayo imekusanya pointi 41 mpaka sasa.

# Michezo

Jumatatu Januari 27, 2025

Nipashe




Arteta akerwa na kadi nyekundu UKURASA 22

SAFI HIYO...




Augustine Okejepha (kushoto), akimpongeza Ladack Chasambi, kwa kuifungia timu yao bao la pili wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Kilimanjaro Wonders kwenye mechi ya raundi ya tatu ya michuano ya Kombe la FA, iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Ramovic apata pakuzungumzia

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Copco FC na katika mchezo wa raundi ya tatu Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema kazi iliyobaki sasa ni kushinda kila mchezo wa mbele yao kwa timu yoyote ile watakayokutana nayo, bila kujali ni ndogo au ya daraja la chini.



Akizungumza juzi, baada ya kumalizika kwa mchezo huo uliopigwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Ramovic, alisema tangu mwanzo aliwaambia watu kuwa hadharau timu yoyote, hivyo kipigo hicho kimewastahili Copco na ataendelea na utaratibu wa kutoidharau timu yoyote ile, iwe kwenye Ligi Kuu au Kombe la FA.

"Tumecheza vizuri kwenye huu mchezo, tumeingia hatua ya robo fainali, hatuangalii timu ndogo, timu ya daraja la chini, au tumepangiwa na mpinzani wa aina gani, tunajiangalia wenyewe.

"Watu wasidhani kuwa tumefunga mabao kirahisi, unaona jinsi gani ilivyokuwa timu nzuri na iliziba mianya kipindi chote cha kwanza, cha pili matokeo yaliamuliwa kwa sisi kubadilisha mfumo , pia uwezo na kipaji cha mchezaji mmoja mmoja, tutajaribu kuendelea na makali haya kwa yeyote yule atakayekuja bila kujali ipo chini ya msimamo wa Ligi Kuu au ipo daraja la chini Kombe la FA," alisema kocha huyo.

Ushindi huo unakuja wiki moja tu baada ya kushindwa kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilipolazimishwa sare dhidi ya MC Alger ya Algeria na kuishia nafasi

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yatoa fundisho FA

### Yapeleka gharika ya mabao kwa Kilimanjaro Wonders huku ikiweka rekodi kwa bao la...

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Simba, imesonga mbele Kombe la FA, baada ya kuichakaza Kilimanjaro Wonders mabao 6-0 katika mchezo wa raundi ya tatu ya michuano hiyo kusaka bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

**Ushindi huo ulikuwa ni kama kuwajibu watani wao wa jadi ambao Jumamosi iliyopita iliikandika Copco FC mabao 5-0, kwenye uwanja huo huo wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam ikiwa ni mechi nyingine ya kombe hilo.**

Simba ilianza biashara asubuhi, kabla ya dakika moja kutimia, walipoanzisha mpira bila wapinzani wao kugusa wakaukwamisha mpira wavuni.

Alikuwa ni Valentin Nouma, ambaye baada ya gonga mbili, aliambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto na kupiga krosi iliyounganishwa kwa mguu na Velentino Mashaka sekunde ya 23 tu tangu mpira kuanza.

Ladack Chasambi alifunga bao la pili dakika ya nne ya mchezo baada ya wachezaji wa Simba kupasiana karibu na lango la wapinzani wao, mfungaji awali alipiga pasi ya kisigino kwa Awesu Awesu, ambaye naye alipeleka pembeni, wingi ya kulia, kabla ya David Kameta kupiga krosi iliyounganishwa naye.

Bao la tatu liliwekwa ndani ya nyavu na beki wa Kilimanjaro Sebastian dakika ya tisa, baada ya kukabiliwa na shuti la Valentine Nouma.

Mpira ulitoka kwa Mzamiru Yassin, ambaye alimpenyezea Joshua Mutale, aliyepiga pasi ya kisigino kwa Nouma, ambaye shuti lake lilimbabatiza beki huyo na kumpoteza maboya kipa, Farances Kizuguto.

Mutale alifunga bao la nne dakika ya 20, baada ya kipa Kizuguto kuupiga pembeni kwa mabeki wake, lakini wakachelewa kuupitia na kuujaza wavuni.

Mabao hayo yalidumu hadi mapumziko, huku kipa wa Simba Ally Salim, akiwa kama yuko likizo licha ya kujaribiwa na mipira miwili ya hatari, alipookoa shuti la Hamis Ramadhani, kabla ya Playgod Nassari kukosa bao la wazi, baada ya kuukuta mpira uliorudishwa na Nouma kwa kipa wake, lakini haukwenda mbali.

Shuti lake akiwa karibu na lango, halikuwa na shabaha, mpira ukatoka nje.

Kipindi cha pili, angalau vijana wa Kilimanjaro Wonders, walionekana kuamka, lakini ni baada ya kufungwa bao la tano mara tu baada ya kuanza kipindi hicho, dakika ya 48 lililowekwa wavuni kwa kichwa na Steven Mukwala, likiwa ni bao pekee lililofungwa kwa staili hiyo kwenye mechi hiyo.

Mpira ulianzia nyuma kwa Abdulrazack Hamza, ambaye alipeleka pembeni kwa Duchu, aliyeambaa kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi ya juu, mfungaji akiruka na kuunganisha, akimwacha kipa, Kizuguto, akiruka bila mafanikio.

Mukwala alikuwa ameingia kuchukua nafasi ya Mashaka, ambapo mbali na mchezaji huyo, wengine walioingia ni Edwin Balua badala ya Augustine Okejepha, Kelvin Kijili naye akiingia badala ya Hamza.

Baada ya mabao hayo, wachezaji wa Simba walionekana kuridhika na kupunguza kasi yao, hali iliyowafanya Kilimanjaro Wonders kuanza kujinafasi

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >